# NAFASI YA DINI KATIKA NDOA: TATHMINI YA *UTENGANO NA PARADISO*

NA

MUHANDA BITINYU HOWARD

University of NAIROBI Library
0479826 0

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Chuo kikuu cha Nairobi

2011

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

______________________ 5/11/2011

MUHANDA BITINYU HOWARD Tarehe

Mtahiniwa (C50/78807/2009)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu cha Nairobi

______________________ 5-11-2011

DKT. EVANS MURAGE MBUTHIA Tarehe

MSIMAMIZI

______________________ 7/11/2011

DKT. FRANCIS MUSYOKA Tarehe

MSIMAMIZI

## TABARUKU

Kazi hii namtaburukia marehemu baba yangu Festus Bitinyu Muhanda kwa kunitakia mema maishani na kwa kunitunza kwa mapenzi ya mzazi hadi alipoiaga dunia. Aidha namshukuru kwa kunitakia hili ijapokuwa hakuishi kuliona.

Na kwa mama yangu mpendwa Agnetta Muhanda, ni mama aujuao uchungu wa mwana.

## SHUKURANI

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kutimiza utafiti huu katika somo la kiswahili.

Pili nawashukuru wasimamizi wangu Dkt. Evans Mbuthia na Dkt. Francis Musyoka kwa kunishughulikia kwa moyo wao wote ili kufanikisha utafiti huu. Ningependa pia kuwashukuru waalimu wangu wote kwa kufanikisha masomo yangu, shukurani tele zimwendee Dkt. Iribe Mwangi kwa kuhakikisha kuwa masomo haya yamekamilika bila shida nyingi.

Pia namshukuru mke wangu kwa kuwatunza watoto wetu peke yake nilipozama masomoni. Nawashukuru pia wazazi wangu kwa kunipa moyo Katika kufanikisha masomo yangu.

Pia shukrani tele ziwaendee wanafunzi wenzangu wote walionitia moyo katika masomo haya.

# MUHTASARI

Utafiti huu umeshughulikia nafasi ya dini katika ndoa na vile uhusiano huu wa dini na ndoa unavyomwathiri mwanamke katika jamii.

Sura ya kwanza ni tatizo la utafiti, madhumuni, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi ya nadharia, na njia za utafiti.

Sura ya pili imeshughulikia athari ya dini ya kikristo katika taasisi ya ndoa na maswala mengine yanayoibuka katika *Paradiso* (2005).

Sura ya tatu imeshughulikia athari ya dini ya Kiislamu katika taasisi ya ndoa na masuala mengine yanayoibuka katika Riwaya Ya *Utengano* (1980).

Sura ya nne ni hitimisho na mapendekezo kuhusu utafiti wa baadaye wa kazi kama hii.

## YALIYOMO

**Ukurasa**

Ungamo ...................................................... ii
Tabaruku ...................................................... iii
Shukrani ...................................................... iv
Muhtasari ...................................................... v
Yaliyomo ...................................................... vi
**SURA YA KWANZA**
1.0 Utangulizi ...................................................... 1
1.1 Tatizo la utafiti ...................................................... 5
1.2 Madhumuni ya utafiti ...................................................... 6
1.3 Upeo na mipaka ya utafiti ...................................................... 6
1.4 Sababu za kuchagua mada hii ...................................................... 6
1.5 Nadharia tete ...................................................... 7
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada ...................................................... 7
1.7 Msingi wa nadharia ya utafiti ...................................................... 10
1.7.1 Ufeministi wa Kiafrika ...................................................... 15
1.7.2 Ufeministi wa Kiislamu ...................................................... 17
1.7.3 Mihimili ya nadharia ya ufeministi wa Kiislamu ...................................................... 19
1.7.4.0 Vipengele muhimu vinavyozingatiwa katika ufeministi wa Kiislamu ...... 20
1.7.4.1 Ubinafsi wa mtu dhidi ya jamaa nzima ...................................................... 21
1.7.4.2 Tofauti za kijinsia katika wajibu wa maisha ...................................................... 21
1.7.4.3 Dini ya Kiislamu imempa mwanamke daraja tofauti kisheria na Mwanamme ...................................................... 22
1.7.5 Chukulizi za kimsingi za ufeministi ...................................................... 22
1.8 Njia za utafiti ...................................................... 23
1.9 Hitimisho ...................................................... 24
**SURAYA PILI**
2.0 Utangulizi ...................................................... 25
2.1 Mtazamo wa ndoa katika dini ya Kikristo ...................................................... 26

2.2 Athari za dini katika ndoa mbalimbali katika riwaya ya *Paradiso* ........................ 30
2.3 Matatizo ya wanawake katika ndoa yanavyosawiriwa katika riwaya ya *Paradiso* ........................ 43
2.4 Hitimisho ........................ 47

**SURA YA TATU**

3.0 Utangulizi ........................ 48
3.1 Athari za dini ya Kiislamu katika ndoa ........................ 49
3.2 Athari za dini ya Kiislamu katika ndoa katika riwaya ya *Utengano* ........................ 57
3.3 Matatizo yanayowakumba wanawake katika riwaya ya *Utengano* ........................ 60
3.4 Hitimisho ........................ 65

**SURA YA NNE**

4.0 Utangulizi ........................ 66
4.1 Hitimisho ........................ 66
4.2 Mapendekezo ........................ 69

Marejeleo ........................ 71

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Fasihi kama taaluma inayotumia lugha katika kuyaangazia masuala mbalimbali yaliyoko katika jamii hujumuisha vipengele vingi ambavyo, aghalabu vinaweza kuchambuliwa katika viwango kadhaa. Miongoni mwavyo ni lugha,wahusika na maudhui.Kwa hivyo ni sharti tuelewe kwamba kila jamii inakitwa kwenye utamaduni wake na hivyo basi,wanafasihi wanahitaji kuyamulika masuala mbalimbali yanayojiri katika jamii wanazoandikia mintaarafu ya maisha ya wanajamii husika. Ni kutokana na mkabala huu ambapo wanafasihi hufumbata tajriba na miondoko ya wanajamii na kisha kupitia kwa kazi ya kubuni, wanatoa maoni,mapendekezo, kashfa na sifa pindi inapotokea haja ya kufanya hivyo, Mlachi (1991). Kwa hivyo utafiti huu wetu unadhamiria kutumia fasihi kutathmini, kuwa dini ina nafasi gani katika asasi ya ndoa kwa kutumia riwaya za kiswahili *Utengano* (1980) na *Paradiso* (2002).Kulingana na Ndungo (1998) kazi za fasihi andishi na simulizi huonyesha asasi za jamii iliyozichipuza, anaafiki kuwa fasihi ni kifaa muhimu cha kutazamia maisha ya jamii na kuwa jamii ni dhihirisho la utamaduni ambao hujumuisha sanaa ya jadi (elimu ya mila na desturi za jadi), dini, matambiko na mengineyo. Nikaha zimewahi kujadiliwa katika kazi mbalimbali ambazo zimetoa picha tofauti kuhusu dini na ndoa. Kuna zile ambazo zinaipa ndoa taswira chanya na nyingine zinaipa taswira hasi,hasi kwa maana ya kwamba zinaionyesha kama asasi yenye madhila mengi.

Kila jamii ina jukumu la kuhakikisha ina muumano mwema na fasihi ndiyo ina jukumu la kuhakikisha muumano huu upo katika jamii. Uhusika wetu katika jamii unaamuliwa na

itikadi na kila jamii ina itikadi zake,haya ni kwa mujibu wa Althusser Louis katika, Billington(1991). Fasihi hudhihirisha na kubainisha hali halisi ya jamii, msanii ni zao la jamii na huchota maudhui yake kutokana na hali halisi zinazomzunguka za kitamaduni, kiuchumi, kijamii, na kisiasa,kwa hivyo kazi ya fasihi hutupa picha kamili ya maisha ya jamii za kisasa. Billington (ibid) anaendelea kusema kuwa mtu anapokiuka hali inayokubalika ya jamii basi huwa ameichafua jamii hiyo anasema kuwa kukiuka maadili katika jamii ni uchafu wa jamii, jamii ndiyo huamua ni yapi adilifu na ni yapi yasiyofaa.Hali hii basi itasababisha uchunguzi huu wetu kuhusu athari ya dini katika asasi ya ndoa katika jamii kwa kutumia fasihi andishi.

Mwanasosholojia Durkheim (1957) anaiona jamii kama mfumo wenye asasi na njia maalum za kutenda na kutumia lugha moja, mambo haya yote huathiri maisha ya wanajamii. Tutaangazia mtazamo wa jamii kuhusu ndoa kwa ujumla na matatizo yanayokumba ndoa katika jamii.

Fasihi husawiri mahusiano ya wanajamii katika shughuli zao za kila siku mahusiano ya jamii huongozwa na kaida na desturi za jamii husika. Suala la ndoa ambalo ndilo msingi wa utafiti wetu ni mojawapo wa mahusiano muhimu ya kijamii kwa kusoma na kusikiliza kazi za fasihi, twaweza kuelewa mengi kuhusu mielekeo, falsafa na mahusiano ya kijamii.

Fasihi yaweza kuonyesha makundi mbalimbali katika jamii yanavyohusiana na vile kati ya mahusiano haya kuna yale makundi yaliyowekwa pembeni na yale yaliyoyatawala mengine katika jamii.Utafiti huu utachunguza kuhusu jinsi mielekeo kuhusu ndoa inavyojitokeza katika fasihi.

Allen(1971) anasema yafuatayo kuhusu ndoa ya Mikidadi na Mayasa Katika utenzi wa Mikidadi na Mayasa,

Ubeti 666 **Akaketi na mayasa**
**Kila siku ni arusi**
**Vitu jinsi jinsi**
**Kila siku huandaa**

Katika ubeti huu inasemekana Mikidadi na Mayasa waliishi kila siku kama kwamba ilikuwa siku ya arusi,katika ndoa yao kila jambo liliwaendea vyema nyakati zote kiasi kwamba, hakukuwa na shida wala madhila yoyote. Kazi kama hizi ndizo zimekuwa kichocheo kikubwa katika utafiti huu,kwani tunataka kuchunguza madhila yanayopatikana katika ndoa na pia kuchunguza anayesababisha madhila haya ni nani, au ni nini kinachosababisha matatizo katika ndoa hizo.

Mwanakupona katika utenzi wake maarufu wa Mwanakupona aliandika mengi kuhusu ndoa, hasa jinsi ambavyo mke alivyopaswa kuwa mnyenyekevu na kumhudumia mume. Beti mbili zifuatazo zinaonyesha msimamo wa Mwanakupona Mshamu kuhusu asasi ya nikahi.

Ubeti 28 **Keti naye kwa adabu**
**Usitie ghadhabu**
**Akinena simjibu**
**Itahidi kunyamaa**

Ubeti 36 **Mpumbaze apumbae**
**Amriye sikatae**
**Maovu kieta yeye**
**Mngu atakulipa**

Kutokana na dondoo lililo hapo juu, Mwanakupona katika utenzi huu anaonelea kwamba,mwanamke anaweza kufanya kila awezalo kumfurahisha mumewe na ikiwa huyo mume atamkosea mke anapaswa kuyaachia Mungu ambaye atamlipia, ni kwa msingi huu ambapo waandishi wengi wamechukulia kuwa tamaduni pamoja na asasi ya dini zinatumiwa kumkandamiza mwanamke.

Robinson na Richardson(1993) wanadai kwamba, ili kuelewa utendakazi wa ubabedume ni muhimu kuelewa asasi ya ndoa kwa kuwa asasi hii ya ndoa ndiyo huendeleza ubabedume, wanazidi kufafanua kuwa, suala la ndoa si uchaguzi wa mtu bali hii ni asasi ambayo imejengwa na jamii ili kuendeleza ubabedume kwa kuzingatia namna wanawake wanavyoingizwa kwenye asasi yenyewe,kumbuka jamii inatawaliwa na wanaume na kumtweza mwanamke kwa hivyo wameijenga ndoa ili kuendeleza ubwana katika jamii.Hata hivyo, dini za Kikristo na Kiislamu hazilazimishi waumini wao kuoa au kuolewa ingawa dini zote mbili zinachukulia ndoa kama asasi muhimu katika jamii.

Mtafiti mwingine tutakayeangalia maoni yake katika sehemu hii ni Gaskof(1971)ambaye anaelezea kuwa, kwa muda mrefu watu wamevitumia vifungu fulani fulani vya Bibilia ili kumnyanyasa na kumdhulumu mwanamke huku wakimwonyesha mwanamume kama binadamu kielelezo.

Mojawapo wa vifungu vya Bibilia ambavyo vimetumiwa visivyo ni kutoka kitabu cha Timotheo ya kwanza kifungu cha pili,kinachosema ya kwamba mwanamke anatarajiwa kujifunza kwa kimya na unyenyekevu, pia mwanamke hakubaliwi kutoa mafundisho wala kuwa na mamlaka juu ya mwanamume kila mara anatakiwa awe kimya kwani hata Adamu aliumbwa mwanzo naye Hawa baadaye. Bibilia inaendelea kusema ya kwamba,

Adamu hakudanganywa bali ni Hawa aliyedanganywa,vifungu hivi vinadhihirisha jinsi Bibilia inaweza kutumiwa kuathiri ndoa kwa kumdhalilisha mwanamke.

Wamitila (2002) anaeleza kwamba asasi ya dini na ndoa hutumika katika kumkandamiza mwanamke.

Mambo mengi yameandikwa kuhusu taasisi hizi mbili, dini na ndoa. Katika utafiti huu wetu tunanuia kuzitazama dini na ndoa kwa jicho pevu na kuona kama kweli kuna mahusiano yoyote kati ya dini na ndoa kwa mujibu wa riwaya zetu za utafiti ambazo ni: *Utengano* na *Paradiso*. Lengo letu kuu ni kuchunguza kama dini ina nafasi yoyote katika ndoa na kudhibitisha kama hali ya mwanamke katika ndoa ni duni kama inavyoonyeshwa katika kazi zilizotangulia na ikiwa ni kweli kuwa dini huathiri ndoa, Pia tunahitaji kuchunguza ni kwa nini wanawake wanajiingiza katika asasi hizi mbili zinazo watesa na kuwanyanyasa.

### 1.1 Tatizo la utafiti

Tatizo la utafiti ni kuchunguza kama kuna mahusiano kati ya asasi ya dini na asasi ya ndoa hasa kwa kumuangazia mwanamke katika riwaya mbili za kiswahili,yaani *Utengano* na *Paradiso*.Kuna haja ya kushughulikia dini katika suala la ndoa kwa kuwa dini huchukuliwa kama dira katika ndoa.Kwa hivyo utafiti huu wetu unadhamiria kutumia fasihi kutathmini, kuwa dini ina nafasi gani katika asasi ya ndoa kwa kutumia riwaya za Kiswahili Utengano (1980) na Paradiso (2002).Watu wanapoingia katika dini huwa wana matumaini mengi ya kupata manufaa kutoka kwa dini, na hata ndoa nyingi hujengwa kwa mhimili wa dini.Katika utafiti wetu tunataka kuchunguza kama kuna uhusiano wowote kati ya asasi ya dini,ndoa na mwanamke katika jamii kwa mujibu wa riwaya teule za Kiswahili.Kuna mengi yaliyoandikwa kuhusu mada ya dini na ndoa,lakini

kuna tafiti chache zilizofanywa kuhusu mada zenyewe katika riwaya ya Kiswahili na hasa kuhusu nafasi ya dini katika ndoa.Hili ndilo pengo hasa tunalotaka kuliziba katika utafiti huu.

### 1.2 Madhumuni ya utafiti

(i) Katika utafiti wetu tunachunguza mahusiano kati ya asasi ya dini na asasi ya ndoa kama ilivyosawiriwa katika riwaya za *Utengano na Paradiso*.

(ii) Kutathmini ufaafu wa nadharia za ufeministi katika kuchanganua nafasi ya mwanamke katika mahusiano haya ya dini na asasi ya ndoa.

### 1.3 Upeo na mipaka ya utafiti

Kazi yetu ni ya kifasihi na tunalenga kuhakiki ikiwa asasi ya dini ina mahusiano yoyote na asasi ya ndoa, Pia kuchunguza nafasi ya mwanamke katika mahusiano haya ya dini na ndoa. Katika utafiti wetu,tutaangalia asasi za dini na ndoa katika riwaya ya *Utengano* (1980) ya S.Mohamed na *Paradiso* (2005) ya J.Habwe. Tunakusudia kuhakiki maudhui ya ndoa na dini na masuala husika kama yalivyoshughulikiwa katika riwaya hizi. Hata hivyo pale itakapolazimu tunaweza kurejelea vipengele vya fani au maudhui mengine mbali na ndoa na dini ili kutilia mkazo swala hili.

### 1.4 Sababu za kuchagua mada hii

Katika utafiti huu,tutashughulikia riwaya mbili ambazo ni *Paradiso*(2005) na *Utengano*(1980). Kazi hizi mbili zina tofauti ya miaka ishirini na mitano katika kuchapishwa kwazo na kwa hivyo tunakusudia kuona kama kuna tofauti kuhusu mahusiano kati ya dini na ndoa kama alivyoandika S.A. Mohamed mnamo mwaka wa 1980 na J.Habwe mnamo mwaka wa 2005. Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni kwamba, riwaya ya *paradiso* haijashughulikiwa,pia riwaya hizi ziliteuliwa kimaksudi ili

riwaya ya *Utengano* iwakilishe dini ya Kiislamu na athari zake katika ndoa na *Paradiso* iwakilishe dini ya Kikristo na athari zake katika ndoa. Kusudi lingine ni kulinganisha ndoa na athari zake katika mfumo wa umwinyi na ubepari. Sababu nyingine ni kuangalia riwaya iliyoandikwa na mwandishi kutoka Tanzania (Utengano) na Kenya(Paradiso). Tungependa kutathmini mahusiano ya dini na ndoa katika nchi hizi mbili kama yana mfanano wowote na nafasi ya mwanamke katika mahusiano haya.

## 1.5 Nadharia tete

Utafiti wetu unaongozwa na nadharia tete kwamba:

(i) Wasanii wa kazi hizi mbili,wamezisawiri asasi za dini na ndoa kama nyenzo zinazotumika katika kumdhalilisha mwanamke.

(ii) Katika kazi hizi dini imeonyeshwa kama tatizo kubwa katika asasi ya ndoa na mwanamke ndiye anayepata dhuluma dini inapoathiri ndoa.

## 1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Kuna mengi yaliyoandikwa kuhusu mada ya dini na ndoa lakini ni tofauti na utafiti huu wetu ambao unashughulikia nafasi ya dini katika ndoa katika riwaya ya kiswahili.

Njogu (1997) amehakiki riwaya za visiwani zanzibar kwa misingi ya nadharia ya ufeministi, tofauti ya kazi ya Njogu na kazi hii yetu ni kuwa yeyé ameangalia tu nafasi ya mwanamke katika riwaya nasi tunaangalia mahusiano kati ya dini, asasi ya ndoa na mwanamke katika riwaya za *Utengano* na *Paradiso*.

Clayton (1978) katika *The Family,Marriage and Social Change* anadai kuwa ndoa ni tukio linalomtoa mtu kutoka hadhi moja kijamii hadi nyingine. Nao Maina(2005) na Osoro (2003)wanaeleza kwamba, ndoa ni mojawapo ya asasi ambazo wanaufeministi wengine wanapigania kwamba zifutiliwe mbali kutoka jamii zetu. Maina na Osoro

wanazungumzia nafasi ya mwanamke katika ndoa kwa hivyo makala yao yatatusaidia kurutubisha kazi yetu.

Wamitila (2007) kwenye mwongozo wa *Mwisho wa Kosa* ameandika kuhusu usawiri wa asasi ya ndoa, katika mwongozo huu, amesema ya kwamba, ndoa imepewa sura mbili, sura ya kwanza ni ile ya kitamaduni inayopangwa na wazazi na ya pili ni ya kisasa ambapo wachumba hujipangia wenyewe. Mwongozo huu utatusaidia katika kulinganisha usawiri wa ndoa katika riwaya ya Mwisho wa Kosa na riwaya zetu mbili tunazozitathmini.

Lisa (1986) katika *The Encyclopedia of Feminism* amezungumzia tawi la Marekani la Ufeministi mnamo mwaka wa 1969 lililotangaza kwamba;hakutakuwa na usawa kati ya wanaume na wanawake hadi pale tutakapovunja asasi ya ndoa. Lisa anaendelea kusema ya kwamba, kwa wanaufeministi wa hapo awali mabadiliko katika ndoa ndiyo yaliyopewa kipaumbele katika kuleta usawa kati ya mwanamke na mwanamume, kwa kundi hili, nikaha ni sawa na kifo kwa mwanamke. Wanadai kuwa mwanamke hupoteza haki zote alizokuwa nazo kabla ya kuolewa, mara tu anapoingia katika asasi ya ndoa kwani mume huwa anamdhibiti pamoja na chochote alichonacho huwekwa katika milki ya mume wake. Kazi hii ya Lisa ni muhimu kwa utafiti huu wetu kwa kuwa inaangalia ndoa kwa misingi ya nadharia za kiharakati za kimarekani nasi tunaangalia ndoa kwa kutumia nadharia ya ufeministi wa Kimarekani ambayo ina uhusiano wa karibu na ile aliyoitumia Lisa.

Katola (2006) katika tasnifu yake ya uzamili aliandika kuhusu udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia ya Kiswahili. Baadhi ya udhalimu aliogundua ni pamoja na:kudharauliwa, kutusiwa, kutishwa, kutawishwa, kuozwa bila hiari, kupigwa na

kunyimwa haki.Kazi yetu ni tofauti na ya Katola kwa kuwa inajikita katika riwaya na jinsi dini inahusiana na asasi ya ndoa kwa kumuangazia mwanamke.

Nyaosi (2006) katika tasnifu yake ya uzamili aliandika kuhusu taswira ya asasi ya ndoa katika riwaya mbili za Kiswahili: *Kiu* na *Msimu* wa *Vipepeo*. Katika tasnifu hii Nyaosi anaangazia dhuluma anazozipata mwanamke katika asasi ya ndoa. Tofauti kati ya kazi yetu na ya Nyaosi ni kuwa tunaangazia riwaya tofauti na alizoangazia na pia sisi hatuangalii tu ndoa bali tunaihusisha na dini.

Chesaina (1987) ameshughulikia jinsi wanawake walivyosawiriwa katika tamthilia za Kiingereza, Kifaransa na Kiswahili. Lugano (1989) ameshughulikia usawiri wa wahusika wa kike katika riwaya nne za E. Kezilahabi, ameonyesha ukataji tamaa katika juhudi za ukombozi wa wanawake. Utafiti wetu ni tofauti na wa Lugano kwa kuwa wetu utaonyesha jinsi fasihi inavyoshughulikia suala la dini katika asasi ya ndoa. Muindi (1990) ametafiti kuhusu usawiri wa wahusika makahaba katika riwaya za Said Ahmed. Kazi yetu ni tofauti na ile ya Muindi kwa vile inaangalia jinsi hali ya ndoa inavyochorwa katika riwaya teule na jamii za kiafrika kwa ujumla hasa ikiangazia viongozi wa dini ambao ndio wanatarajiwa kuwa vielelezo bora katika jamii na vile wanavyohusiana katika ndoa zao.Kazi ya Muindi ni muhimu katika urutubishaji wa kazi hii yetu kwa vile wakati mwingine ukahaba ni shida anazozipitia mwanamke katika jamii na hili ndilo suala tunaloliangazia.

Mule (1991) ametafiti kuhusu mitazamo ya waandishi wa kike kuhusiana na wanawake katika tamthilia za Kiswahili, kazi yetu ni tofauti kwa vile inatafiti kuhusu suala la ndoa na changamoto zake katika riwaya zilizoandikwa na wanaume.

Momanyi (1998) ameangazia jinsi ushairi wa Kiswahili unavyomsawiri mwanamke kazi yetu haihusu jinsia ya kike tu bali muono wa jamii kwa jumla na mahusiano kati ya dini na ndoa.

Kimani (2003) anamulika jinsi kazi teule za fasihi zinavyoonyesha maudhui ya dhuluma kwa wanawake, tofauti kati ya kazi hii na yetu ni kuwa sisi tunaangazia ndoa kwa muktadha wa kidini.

## 1.7 Msingi wa nadharia ya utafiti

Nadharia ni kigezo cha kutathminia jambo, utafiti wowote wa kiusomi huhitaji nadharia mwafaka itumikizwe ili kuufanikisha (Wafula na Njogu 2007:2). Utafiti wetu unahusisha saula lenye mawanda mapana mno.Suala la ndoa ni la kimila katika jamii na changamoto zake huathiri jamii kisaikolojia, kisosholojia na hata kidini. Utafiti huu basi utatumia nadharia za kifeministi ili kukidhi mahitaji yote ya mada inayoshughulikiwa.Ufeministi ni dhana inayotokana na neno la Kilatini "Femina" lenye maana ya mwanamke, dhana hii inarejelea uwakilishaji wa kazi za wanawake kufuatana au kuambatana na imani ya usawa wa kijinsia. Huu ni mwamko wa wanawake unaolenga kupigania kukomeshwa kwa udhalimu dhidi ya mwanamke kwa njia yoyote ile. Tuki (1986) wanaeleza kwamba ufeministi ni nadharia inayopendekeza kupiganiwa kwa ukombozi, haki na usawa kati ya wanawake na wanaume. De Beauvoir (1949) anaishambulia asasi kama utamaduni akidai kuwa unamwangalia mwanamke kama kitu hasi na cha kando huku ukimchukulia mwanamme kama binadamu kielelezo.Wamitila (2002) anaongezea kuwa ndoa ni asasi mojawapo ya kitamaduni inayoendeleza ukandamizaji wa mwanamke, anatilia nguvu wazo hili kwa kueleza kuwa asasi kama dini inatilia mkazo au nguvu mpya tamaduni

dhalilishi dhidi ya mwanamke kwa kuziwekea mihimili ya matamko ya kidini. Kwa mujibu wa *The New Columbia Encyclopedia* ufeministi unaelezwa kama vuguvugu linalopigania usawa kati ya wanawake na wanaume kisiasa, kijamii na kielimu. Vuguvugu lenyewe liliasisiwa katika nchi za Uingereza na Marekani ambapo kwa miaka mingi wanawake walichukuliwa kuwa dhaifu kimaumbile na kiakili, nyakati hizo sheria za dini ziliidhinisha kutawaliwa na kudunishwa kwao, inazidi kufafanua kuwa, nyakati hizo mwanamke hakuruhusiwa kuandikisha kwa jina lake milki yoyote ile au kufanya biashara yoyote ile, pia mwanamke hakuwa na uwezo wa kuhusiana na hali ya watoto wake na mali yake mwenyewe.

Kazi ya Wollstonecraft, *A Vindication of The Rights of a Woman* (1792) ilisisitiza kuwepo kwa usawa wa haki na nafasi za kikazi katika hali zote za maisha kati ya wanawake na wanaume. Hapo awali kulikuwepo na jitihada mbalimbali za kupigania usawa wa kijinsia.Katika nchi ya Ufaransa,wakati wa mapinduzi maarufu ya nchi hiyo mnamo mwaka 1789 hadi 1795 katika kilichojulikana kama "Msimbo wa Napoleon "(code of Napoleon) ambapo wanawake waliandamana kukataa kushushwa kwa hadhi yao pale Napoleon aliposema kuwa akili za wanawake ni dhaifu zikilinganishwa na zile za wanaume na hivyo walihitajika kupewa elimu ya kiwango cha chini na walifaa kufanya kazi za viwango vya chini kama ushonaji.

Kule Marekani ya Kaskazini wanawake kama vile, Abigail Adams na Mercy Otis Warren walikuwa wamewataka marais George Washington na Thomas Jefferson kuongeza kifungu cha ukombozi wa wanawake katika katiba ya nchi yao bila mafanikio. Hata hivyo inasemekana vuguvugu la ukombozi wa wanawake lilianza hasa katika mwaka wa 1848 wakati Elizabeth Lady Stanton, Lucrecia Coffin Mott na wanawake wengine

walipofanya mkutano wa Senecca Falls-New York,walipotangaza matakwa yao ya kuwa na uhuru kwa wanawake wote, pia walidai wanawake wapewe usawa kisheria, masomo ya kutosha,nafasi sawa ya kufanya biashara, usawa wa kupata fidia na haki ya kukusanya ujira na kupiga kura.

Mbatiah (2000) anaeleza kwamba, ufeministi ni nadharia ya kifasihi ambayo kazi yake kuu ni kutetea haki za wanawake dhidi ya ukandamizaji katika jamii iliyo na mfumo uliodhibitiwa na mwanamme.

Wamitila (2003) anaeleza nadharia ya kifeministi kama iliyowekewa msingi na msukumo katika kupigania ukombozi wa mwanamke kutokana na pingu za kiutamaduni, kijamii, kidini, kisiasa na kiuchumi. Nadharia hii inachunguza msimamo na itikadi ya kiume ambayo imekuwako kwa kipindi kirefu. Pia nadharia hii hushambulia mitazamo ya kiume kuhusu namna wanawake wanavyotarajiwa kuishi.

Nadharia ya ufeministi kwa maoni ya Njogu (1999) inakinzana na mikabala ya kuumeni ambayo huwa inaonekana kuwa ya kuwapendelea wanaume na kuwabagua na kuwanyanyasa wanawake. Njogu (ibid) ametoa sifa sita za nadharia hii:

(i) Nadharia ya ufeministi hutumia fasihi kama jukwaa la kuelezea kwa uyakinifu hali inayomkumba mwanamke ili iweze kueleweka na watu wengi.

(ii) Hii nadharia inanuia kusawazisha wanadamu kwa upande wa utamaduni na umenke, inapigania jamii mpya yenye msingi katika amali za binadamu bila kujali maumbile. Ubinadamu unapewa nafasi ya kati.

(iii) Mtazamo huu vile vile unajaribu kuwahamasisha watungaji wa kazi za sanaa ili wawe na wahusika wa kike ambao ni vielelezo, wenye uwezo na wanaoweza kuigwa. Wahusika hao watakuwa na nguvu za kijamii hata bila kuwategemea wanaume.Pia kisaikolojia wawe ni wanawake wanaojiweza na kujiamini wala wasiwe wanajihisi kama wanaudhaifu kwa ajili ya umenke wao.

(iv) Nadharia hii hukuza na kuendeleza umoja wa wanawake kama kundi linalodhulumiwa, wanawake wanahimizwa kuungana.

(v) Shabaha ya mtazamo huu ni kuamsha na kuzindua mwamko miongoni mwa wanawake ili wawe watendaji zaidi na washiriki ipasavyo katika ukombozi wao wenyewe,mkabala huu unatilia mkazo kauli ya utendaji na wala si ya upokezi.

Nadharia hii inatilia maanani na kusisitiza umuhimu wa kuvumbua na kuweka wazi kazi zilizotungwa na wanawake ambazo zimepuuzwa kwa sababu ya utamaduni unaompendelea mwanamme. Kwa mfano fasihi ya kike inafufuliwa katika baadhi ya kazi za fasihi ya Kiswahili.

Webster (1970) akiuelezea msimamo wa mwandishi maarufu wa masuala ya kifeministi Viginia Woolf katika kazi yake *A room of One's Own* (1928:75) anadai "ukosefu wa waandishi wa kike unatokana na hali zao za maisha kwa kukosa uwezo wa kifedha na kwa ujumla wanahitaji kuhudumia mahitaji ya wanaume…"

Mizozano ya kijinsia inaelezewa vyema sana nao Dora(1925) na Webster(ibid) wanapoelezea kuwa, katika ulimwengu wa leo,ugomvi katika ndoa kama ilivyo kwenye vita,ni mwingi kiasi kwamba, hauwahusu mtu na mtu mwingine bali unahusisha makundi ya jinsia na matabaka yote ya jamii. Webster anazidi kufafanua kwamba, dharau kwa mwanamke inaonekana wazi kwani mara nyingi mtu anapohusishwa na sifa za kiume huwa inachukuliwa kama amejihusisha na hali chanya ilhali kuhusishwa na sifa za kike huonyesha hali hasi.

Mwanaufeministi maarufu Simone de Beauvoir katika kitabu chake maarufu cha-*The Second Sex* (1949) anaeleza bayana namna ambavyo mwanamke anadunishwa katika asasi ya ndoa,anadai kuwa mke huchukuliwa kama msaidizi wa mume na huwa kama

bidhaa machoni mwa mwanamme,anaendelea kusema kuwa,mwanamke akiwa mtoto hudhibitiwa na babake na anapokuwa mtu mzima babake humkabidhi kwa mwanamme mwingine ambaye ni mume wake katika ndoa ili akamdhibiti zaidi.Ubidhaishaji huu ndio unaowafanya wanaume wengine kuoa wake wengi. Beauvoir anazishambulia baadhi ya taasisi ambazo zinachangia kumdhalilisha mwanamke nazo ni dini, ndoa na utamaduni.

Ogundipe (1994) anaeleza kuwa wanawake hupewa majukumu hasi katika jamii kama uchawi na wanaume huchukuliwa kama wenye nguvu na werevu, hali kama hizi huchangia kwa kiwango kikubwa kumdhalilisha na kumtweza mwanamke

Tuttle (1986) anadai kwamba ufeministi unaibuka kwa kuwa kuna dosari ya namna ambavyo mwanamke anavyochukuliwa.

Kuna matawi mengi ya kifeministi kwa mfano, Ufeministi wa Kiislamu,Ufeministi wa Kikristo, Ufeministi wa Kiharakati, Ufeministi wa watu weusi, Ufeministi wa kimaksi na kadhalika. Kwa kuwa kuna aina nyingi ya ufeministi, na ufeministi huu wote unapigania uwezo wa mwanamke,sisi katika utafiti huu wetu tutajikita katika aina mbili za ufeministi kwanza ufeministi wa Kiafrika na ufeministi wa Kiislamu sababu za kuteua ufeministi wa Kiafrika ni riwaya ya *Paradiso* ambayo tunaitathmini katika utafiti huu wetu ina mizizi yake katika tamaduni za Kiafrika kwa hivyo ni vyema kuangalia mtazamo wao kuhusu ndoa na mwanamke kinyume na dini ya kiislamu ambayo ina misingi yake kwa karibu na tamaduni za Kiafrika.

Katika kuchunguza dini ya kiislamu na uhusiano wake na ndoa tutatumia ufeministi wa Kiislamu unaohusika na ukombozi wa mwanamke katika dini ya Kiislamu aina hii ya ufeministi inahusiana kwa karibu na mada yetu ambayo ni athari ya dini katika ndoa na jinsi athari hii humkandamiza mwanamke. Kwa mujibu wa wanaufeministi hawa, ni

sharti kuwe na usawa kati ya waislamu wote licha ya jinsia zao, wanapigania haki za wanawake katika Nyanja zote za maisha. Kwa ujumla nadharia hii itatusaidia katika utafiti huu wetu kwa vile inajishughulisha na juhudi za kumkomboa mwanamke ambalo ndilo lengo la utafiti huu. Wanaufeministi wa kiislamu wana imani kuwa kubaguliwa kwa mwanamke ndio mzizi wa maonevu yote.

Arki muhimu za nadharia hii zinazoifanya kuwa maarufu ni kama zifuatazo: kwanza, ni ile hali ya mwanamke kuwa duni kisiasa, wanawake na wanaume wote ni wanadamu na wanapaswa kupewa haki sawa.Dhamira nyingine ya wana mtazamo huu ni kufutilia mbali dhuluma zinazoendelezwa na taasisi mbalimbali dhidi ya mwanamke, kwa ufupi nadharia ya ufeministi wa kiislamu inadhamiria kuangazia matatizo yanayowakumba wanawake na kuzua mikakati ya kuwakomboa kutokana na tamaduni kandamizi.

Nadharia ya ufeministi wa kiislamu ni muhimu katika kuchambua fasihi zinazojishughulisha na masuala ya kijinsia katika jamii za Afrika Mashariki. Nadharia hii ina mbinu mpya za kuielewa fasihi na zitakazoifanya iwe ya maana na manufaa kwa utafiti huu kwa kuwa suala hili linalotafitiwa linahusu dini.

### 1.7.1 Ufeministi wa Kiafrika

Maeneo mbalimbali ya kijeografia huchangia pakubwa katika kubainisha sauti mbalimbali za uhakiki wa kifeministi.Kwa mujibu wa Charles E.Bressler(2003:150) Ufeministi umenasibishwa na maeneo matatu ya kijeografia Marekani, Uingereza na Ufaransa. Bressler hataji Afrika ambalo pia ni eneo la kijeografia lenye aina yake ya kifeministi. Wahakiki wa Kiafrika wanaojishughulisha na masuala ya uana wanaelekea

kukubaliana kwamba mkabala wa ufeministi unaafiki zaidi uhakiki wa kazi za kimagharibi kuliko kazi za Kiafrika (Ogundipe-Leslie,1994).

Ingawa mengi hayajafanywa kuhusu ufeministi wa kiafrika, katika utafiti huu wetu tutajikita katika ufeministi wa Kiafrika kwa kuihakiki riwaya ya *Paradiso* kwa kuwa maswala mengi yanayoangaziwa katika riwaya hii ni ya jamii ya Kiafrika na mila na desturi zake ambazo zinamgongano n aza Kimagharibi ambazo zinajitokeza katika dini ya Kikriso. Wahakiki hawa wanamini kuwa jamii asilia (primitive society) haikuwa na ubaguzi kati ya mwanamume na mwanamke. Katika jamii hii, wanawake walifanya kazi za nyumbani za kupika, kuwalea watoto nao wanaume wakawa wawindaji katika juhudi za kutafuta chakula. Hata hivyo kazi za kila mmoja wao hazikudunishwa kama inavyofanyika katika jamii zenye ustaarabu (civilized society). Wanawake wa Kiafrika wanasisitiza zaidi upinzani dhidi ya utamaduni unaomnyima mwanamke nafasi ya kutekeleza malengo yake. Miongoni mwa vitengo vya utamaduni huu ni:-

Kukosa uwezo wa kuchagua kuwa mke au mzazi wa mwanajamii, tohara na ukeketaji wa wanawake, kimya cha kulazimishwa, pia desturi na mila zinazomdhalilisha kama vile kuonewa kwa mwanamke asiyezaa. Millet (1977) anasema kwamba ufeministi wa Kiafrika umetokana na utamaduni katika jamii iliyojikita katika kilimo na ushiriakiano wa kijamii. Umejengeka katika misingi thabiti ya kumuhusisha mwanamke katika shughuli tofauti za kijamii bila kuangalia asasi zinazotawaliwa na wanaume. Ufeministi wa Kiafrika unasisitiza usawa katika shughuli za umma (jamii) na utoaji uamuzi kwa wanawake na wanaume.

Strobel (1980) anauona ufeministi wa Kiafrika kama ambao umekumbana na changamoto (visiki) nyingi kutoka asasi tofauti kwa sababu huwa unataka kujua chanzo cha ubaguzi katika maswala ya kiutawala. Mwelekeo pinzani unasisitiza uongozi wa jinsia ya kiume umeipa changamoto nyingi sana mwelekeo wa ufeministi wa Kiafrika. Steady (1981) anaunga mkono ufeministi wa Kiafrika. Anaueleza kama unaojikita katika misingi inayoangalia majukumu tofauti ya kijinsia kama yanayoegemeana kukamilishana, yenye usambamba na usawa katika kuendeleza jamii. Anasema kuwa ufeministi wa Kiafrika unaweka pamoja maswala ya ubaguzi, uana, tabaka na mielekeo tofauti ya kiutamaduni ili kuleta ufeministi uanaomwangalia mwanamke kama kiumbe lakini sio kiumbe kijinsia. Anaendelea kusema kuwa ufeministi wa Kiafrika unaangalia maswala ya kitamaduni yanayomlemaza mwanamke. Unashughulikia maswala ya kijinsia kwa kujikita katika muktadha wa Kiafrika.

### 1.7.2 Ufeministi wa Kiislamu

Ufeministi wa kiislamu uliibuka katika miaka ya 1890 kama harakati za mabadiliko katika urazini wa watu wenye mizizi yake katika usawa wa waislamu wote, wake kwa waume mahali popote hadharani au faraghani. Nadharia hii imekita mizizi yake katika mafunzo ya dini ya kiislamu yanayoongozwa na Quarani takatifu kama matini ya kimsingi ya kumwongoza mwanadamu. Nadharia hii huwahamasisha watu warudie mafunzo ya Qurani na tafsiri zake kama mwongozo wa maisha halisi. Mbinu muhimu ya nadharia hii ni kumcha mwenyezi Mungu na kukubali mafundisho yake ya uislamu na miktadha muhimu ya hadithi za mtume Mohamadi, kwa hivyo nadharia hii inafuata mwongozo wa Qurani takatifu na ufasiri halisi wa hadithi kama mafunzo

mwafaka. Kwa mwanadamu katika ndoa zitakazokuwa na uadilifu na haki katika uongozi wa umma na katika maisha ya kibinafsi.

Ufeministi wa kiislamu ulijihusisha na mwamko wa wanawake kidini, kijamii na kitamaduni. Wana ufeministi wa Kiislamu (Shar'awi na Nassef) waliazimia kuwa haki za mwanamke zilikuwa haki za kijamii na kwamba mabadiliko na mafanikio ya wanawake katika nyanja za elimu kisiasa na kijami yangepelekea maendeleo ya jamii nzima.

Zainab Al- ghazali (1918) aliasisi shirika la wanawake waislamu lililopinga vikali ufeministi wa Kimagharibi kama kosa lisilo na nafasi katika maisha ya wanawake waislamu.

Msingi wa Kiislamu ulimpa mwanamke haki zake na uhuru katika uchumi, siasa, jamii aila na kibinafsi lengo kuu la chama chake lilikuwa kumhusisha mwanamke muislamu na mafunzo halisi ya dini ili aweze kusoma na kuelewa dini yake na haki alizonazo katika ile dini, alisema mwanamke muislamu yuko nyuma na anatakikana kujiepusha na ujinga huo na kuuondoa mabegani mwake ili aamke jinsi dini yake inavyomuamru (Zainab Al-Ghazali katika Leila Ahmad 1999: 189).Aliamini kuwa mwanamke muislamu anapoitukuza dini au utamaduni wake, tangu utotoni, atakuwa katika urazini wake akijitathmini na kujitukuza na kufahamu thamani yake, katika msingi na uthabiti wa kuutafuta ufeministi katika Uislamu.

Hivyo kuanzia vipindi hivyo vya miaka ya 1920 hadi 1950 ulizuka mchakato wa shughuli za vyama vya wanawake vilivyojishughulisha na usomi na uandishi wa kupigania haki za wanawake kisaikolojia na kijamii hasa katika sheria za hadhi ya kibinafsi katika ndoa (personnel law status) na dhuluma ambazo wanawake wanapata nyumbani.

Nadharia hii ina umuhimu sana katika kufanikisha utafiti huu wetu kwa kuwa masuala ya mwanamke na dini ndio msingi wa utafiti wetu.

### 1.7.3 Mihimili ya nadharia ya ufeministi wa kiislamu

Tunapoitumia nadharia ya ufeministi wa kiislamu katika kuchunguza utamaduni wa mwanamke mswahili, makala hii inaangazia ukweli kuwa utamaduni wa mwanamke mswahili ni jibu, nyenzo na sitara inayotumika kuuelewa, kuuheshimu na kuuhakiki utamaduni huo. Nadharia hii inachangia na kuuwezesha utamaduni huu kuwapa maisha bora zaidi, unaowafunza wanawake wa sasa na vizazi vijavyo mila na desturi bora zinazohitaji kuigwa na kuhifadhiwa. Tamaduni nyingine zitajifunza kutokana na utamaduni wa waswahili. Nadharia hii inatuwezesha kuiumba jamii inayowezesha wanawake wasome bila vizuizi na wasababishe maendeleo katika nyanja zote za kijamii na kimaisha. Maendeleo ya ufeministi wa kiislamu katika taaluma ni kuangazia utamaduni wa mwanamke mwafrika ili aweze kutathmini nafasi yake katika utamaduni wa kiislamu na nia ya uislamu kumhusu mwanamke katika jamii. Ni jukumu la yeyote yule kutumia mihimili ya ufeministi huu katika kuboresha maisha ya mwanamke muislamu ambayo yanadhalilishwa na utamaduni wa waswahili ambao umepitwa na wakati, nia ya kuingiza utamaduni huu katika dini ya kiislamu ni kupotosha waislamu na kuwadhulumu wanawake ambao kwa muda mrefu wamenyanyaswa kwa kizingizio cha dini. Wanaume sambuli ya akina Maksuudi wanahitaji kuelimishwa kuwa dini ya kiislamu inataraji haki za mwanamke ziheshimiwe na kuwe na usawa kati ya mke na mume. Kupitia kwa mafunzo tunayoyapata katika riwaya hii ni kuwa mwanamke ni nguzo muhimu katika jamii na mume anayeijenga nyumba yake kwa kumnyanyasa mwanamke,nyumba ile huanguka na kusambaratika kama ilivyosambaratika nyumba ya

Maksuudi. Nao wanawake wanapaswa waelimishwe kuhusu haki zao kama inavyodhihirika katika Kurani Tukufu.Inajitokeza bayana katika riwaya hii ya Utengano kuwa mwanamke ananyanyaswa kwa sababu nyingi zikiwemo kumuabudu mwanamume na kumuangalia kama miungu fulani, swala la jaala na majaliwa limekita mizizi miongoni mwa wanawake waislamu kama akina Tamima ambao hawajaribu hata kidogo kujinasua kwenye dhuluma wanazozipitia katika mikono ya wanaume, hawa ufikikiria kuwa manyanyaso haya yalipangwa na mwenyezi mungu. Kupitia kwa ujasiri wa Biti Kocho inajitokeza kuwa wanaume kama akina Maksuudi wanaweza tu kurekebika wakikabiliwa na ujasiri wa mwanamke,msimamo wetu ni kuwa wanawake lazima wasimame kidete na kuwakabili wanaume haini kama akina Maksuudi; Biti Kocho na Kazija wamejaribu na kufaulu kuwakomesha wanaume hawa, pia ni vyema wanawake waungane ili waboreshe maisha yao kiuchumi kwa sababu kuwategemea wanaume kiuchumi ndio chanzo cha matatizo yao. Farashuu anadhihirisha ili kwa kuanzisha biashara ili ajikimu kimaisha bila kumtegemea mwanamume.

### 1.7.4 Vipengele muhimu vinavyozingatiwa katika ufeministi wa kiislamu

Kwa mujibu wa mwanaufeministi wa kiislamu Al Faruqi 2003,nadharia hii ina vipengele vya kimsingi vitano ambavyo sharti vizingatiwe katika ufasiri wa fasihi ya kiswahili.

1.7.4.0 Mfumo mzima wa familia/aila

Tunapochunguza jamii zetu za kiafrika, misingi ya dini ya kiislamu inapendelea uhusiano Jamaa wote badala ya aila ndogo (nuclear family) au ndugu wa karibu. Waislamu wanaamini kwamba uhusiano wa jamaa wote husaidiana katika shughuli za ndoa, urithi na kutegemeana katika maisha. Kutokana na maelezo haya inafaamika kuwa swala la

utawa haliungwi mkono na mtazamo huu wa ufeministi wa kiislamu. Uzuri wa kuiangalia jamaa kwa upana wake upo kwa sababu ndoa huongozwa katika misingi ya uadilifu na mapenzi yenye umoja na amani,jamaa yote husaidia kujenga ukuruba katika shida, ushauri na huruma hupatikana bila malipo,misukosuko katika ndoa husuluhishwa kwa urahisi. Haya yote yangezingatiwa katika jamii ya akina Maksuudi katika riwaya ya Utengano maisha yangekuwa tofauti na vile yalivyotokea.

1.7.4.1 Ubinafsi wa mtu dhidi ya jamaa nzima

Nadharia hii inashadidia umuhimu wa matakwa ya jamii yawe sambamba na yale ya mwanamke, yaani tunategemeana na tunahitajiana. Kwa hivyo lazima tushirikiane,ili kusitokee mgongano ni heri mwanamke kukidhi hoja za kijamii kabla ya zake binafsi.

1.7.4.2 Tofauti za kijinsia katika wajibu wa maisha

Ufeministi wa kiislamu unaamini kuwa kila jinsia ina dhima yake katika jamii ambazo zinaheshimiana na kutegemeana. Katika kurani Mwenyezi Mungu hatofautishi baina ya mwanamke na mwanamume katika imani zao (Quran 33:35 na 16:97) katika sura hizo tofauti iliyopo kati ya mke na mume ni katika shughuli na wajibu wao katika jamii. Haya huambatana na tofauti za kifizikia kati ya mwanamke na mwanamume katika shughuli za uzazi na malezi ya watoto.Mume anawajibika kiuchumi kumwangalia kwa hali na mali mkewe wakati huo ili waweze kuilea jamii yenye malezi bora kiimani na kihaki na jamii yenye uadilifu. Huku sio kumdhalilisha mwanamke bali ni kuendeleza jamii.

1.7.4.3 Dini ya kiislamu imempa mwanamke daraja tofauti kisheria na mwanamume

Mwanamke anajitambulisha kibinafsi tangu kuzaliwa hadi hatima yake,hali hiyo inamwezesha mwanamke kufanya kazi,biashara na kumiliki ardhi yake au mali yake.Ndoa haimuzuii na haimpokonyi hadhi hiyo wala haimlazimishi kubadili jina na kuchukua la mumewe baada ya kuolewa(Quran5:83 na 24:2)Ufeministi wa kiislamu unaungana mkono kikamilifu na hali hiyo kwani unampa mwanamke nafasi na uhuru wa kujiendeleza kimaisha.

### 1.7.5 Chukulizi za kimsingi za Ufeministi

Kwa jumla,vipengele au chukulizi za kimsingi za ufeministi ni pamoja na:

(i) Jamii ambayo imetawaliwa na mwanaume inaongozwa na itikadi ya kibabedume imerithishwa turathi na thamani fulani kutoka kizazi kimoja hadi kingine na kuishia kuwa chanzo cha kudumu kwa mfumo huu katika jamii kwa kipindi kirefu. Kwa kuendeleza fikra hizi (za unyonge wa), jamii inaishia kuakisi mawazo kama ya Aristotle aliyesema "Kiumbe wa kike yuko alivyo kutokana na upungufu fulani"pamoja na st.Thomas Aquinas aliyesema kwamba wanawake ni wanaume wasiokamilika.

(ii) Kwa kukubali itikadi na fikra kuwa mwanamke ni mnyonge,jamii zinamsawiri mwanamke kama kiumbe duni na huendeleza mawazo haya katika sawia mbalimbali za jamii na kwa njia hiyo kuidhinisha udhalilishaji wa wanawake.

(iii) Wanaufeministi wangependa kuona jamii ikitambua makosa ya mkabala huu au itikadi ya ubabedume.Hali hii inaakisiwa na fasihi na sanaa katika jamii ambayo imemsawiri mwanamke kwa kutumia kwa kutumia taswira maalum na funge

kama *malaika,kahaba,mlezi,mhudumu wa baa,mke wa nyumba,asiyetumia akili nk.* Wanawake wanapaswa kujikomboa kutoka kwa usawiri huu hasi na kujieleza kwa njia chanya.

(iv) Ili kuweza kujikomboa kutokana na hali hasi au mfumo unaokandamiza *wanawake* (sio lazima kila mfeministi awe mwanamke) wanapaswa kuzichanganua kazi za fasihi zinazothaminiwa kama kazi muhimu na kuonyesha jinsi taswira duni zinavyochangia katika kuendeleza utamaduni wa kukandamiza. Wanapaswa kupambana na ubabedume kuihusu jinsia yao.

(v) Wanawake wanatakikana kuwazia upya sehemu inayounda kazi kule katika fasihi,kutathmini uzoevu au tajriba ya wanawake na jinsi inavyojitokeza katika maandishi ya kifasihi na kuuchunguza usawiri na uwasilishaji mzima wa wahusika wa kike katika kazi za fasihi ambazo zimeandikwa na wanaume.

(vi) Hudadisi na kushambulia uwasilishaji wa mwanamke kama *wingine* na huibua masuala na mijadala kama tofauti kati ya mwanamke na mwanaume ni suala la kibiolojia au linahusishwa na miundo ya kijamii.

**1.8 Njia za utafiti**

Huu ni utafiti wa kifasihi na kwa sababu hii,kazi nyingi itafanyika maktabani. Tunalenga kupitia vitabu na majarida mengi iwezekanavyo kuhusiana na mada yetu ya utafiti.

Pia tutapitia kazi mbalimbali zilizoandikwa kuhusiana na nadharia tunayoitumia katika uhakiki huu wetu. Njia nyingine tutakayotumia ni mazungumzo ya ana kwa ana na wataalamu mbalimbali wa fasihi kuhusu mada yetu ya utafiti.

## 1.9 Hitimisho

Katika sura hii tumetanguliza na kueleza madhumuni ya utafiti wetu na upeo na mipaka ya utafiti huu. Pia tumeeleza sababu za kuchagua mada hii na nadharia tete. Tumeeleza pia misingi ya nadharia ambayo itatuongoza katika utafiti huu na njia za kutumia katika utafiti.

# SURA YA PILI

## 2.0 Utangulizi

Dini ambayo ni asasi mojawapo muhimu ambayo utafiti huu unaangazia imeelezwa kwa fasiri mbalimbali.Kulingana na *Oxford Advanced Leaners Dictionary* (1998:988) dini inaelezwa kama "Imani ya kuweko kwa Mungu au miungu ambao wameuumba ulimwengu na kumpa binadamu matumaini ya roho ya kuishi baada ya kufa kwa mwili" (Tafsiri yetu). Naye Coser (1963:276) anaeleza kuwa dini ni mkusanyiko wa imani,desturi na asasi ambazo binadamu katika jamii zote zinazojulikana wamezizua kama majibu kwa zile sehemu za maisha wanazohisi haziwezi kueleweka na kutawaliwa na akili razini zao. Wakristo katika Bibilia na waislamu katika Qurani takatifu hufasiri dini kama imani kiumbe/viumbe wenye nguvu kuliko waumini. Utafiti huu unashughulikia athari zinazoletwa na dini katika ndoa na matatizo wanayoyapata wanawake katika ndoa zilizoathirika. Ni vyema kuziangazia aina mbalimbali za ndoa nchini Kenya na mtazamo wa wanajamii kuhusu ndoa.Kulingana na Kimondo, sheria za Kenya huwapa mume na mke wajibu na haki mbalimbali, katika ndoa, kwa mfano katika dini ya Kiislamu ni wajibu wa mume kumtunza mkewe au wakeze kama ni wengi hili linabainisha kuwa uislamu unaruhusu kuoa mke zaidi ya mmoja.pia katika dini hii mume ndiye kiongozi wa ndoa na ana haki hata ya kumdhibiti mkewe kutenda mambo fulani, mke anatarajiwa kuwa mwaminifu kwa mumewe.

Haki ambayo mke aliyo nayo katika dini hii ni ya kudai mahari na talaka. Sheria za kiraia nchini nazo pia huwapa mke na mume majukumu tofauti, mabadiliko ya katiba yamekuwa afueni kwa wanawake kwa kuwa hata mume lazima amjulishe mkewe ikiwa anataka kuoa mke mwingine, pia wakati wa talaka mali hugawanywa kati ya mke na

mume. Sheria zinawapa mume na mke majukumu ya kulea watoto kwa pamoja, pia kisheria kuna umri ambao yoyote anakubaliwa kufikisha ili aoe (miaka 18).

Jamii nyingi nchini Kenya zinazingatia mila na desturi za jadi katika masuala ya ndoa,kwa mfano katika jamii ya waluo mwanamume anakubaliwa kuoa wake wengi, mke akifiwa na mume analazimishwa akubali kurithiwa na pia mwanamume anaweza kuoa ndugu wa kike kutoka jamii familia moja nk.

**2.1 Mtazamo wa ndoa katika dini ya kikristo**

Ukristo ulienea katika maeneo mengi ya Afrika wakati wa ukoloni na kwa sababu hii waafrika wengi ambao walikuwa na utamaduni wao walianza kuchanganya dini na utamaduni. Tukiangalia mtazamo wa dini ya Kikristo kuhusu ndoa tunapata kuwa waumini wengi hawatofautishi tamaduni za kijadi na mafunzo ya Bibilia.Katika dini ya kikristo ndoa ya mke mmoja tu ndiyo inayotambuliwa na kukubaliwa kama halali machoni mwa mwenyezi mungu,pia ndoa kwa kuwa imechukuliwa kama taasisi muhimu wakristo huthamini ndoa iliyofungamanishwa na padre kanisani. Ndoa huchukuliwa katika dini ya Kikristo kama uhusiano ulioidhinishwa na mwenyezi mungu wakristo wanaamini kuwa uhusiano wa ndoa unahitajika kudumu katika maisha yote ya mume na mke.

Bibilia inasema katika kitabu cha Marko mlango wa 10 mstari wa 11,inasema "mwanamume ambaye anampa mkewe talaka na kuoa mke mwingine anachukuliwa kama anayefanya uasherati na huyu mke aliyemchukua". Vilevile ukiendelea kusoma katika mstari wa 12, "Mke anayempa mumewe talaka na kuolewa na mume mwingine, machoni mwa mungu huchukuliwa kama anayefanya uasherati na mume huyu mwingine." Kifungu hiki kinadhihirisha vile wakristo wanavyoichukulia ndoa na suala la

talaka tofauti na wengine. Wakristo huchukulia kwamba Mungu ndiye anayewaunganisha mume na mke katika ndoa na hawafai kutengana, uhusiano wa ndoa unalinganishwa na uhusiano wa yesu na kanisa, madhehebu mengi ya wakristo hudhamini sana asasi ya ndoa ndiposa yeyote anayetaka kuongoza kanisa lazima awe kielelezo kwa kuwa na mke aliyeoa kwa njia ya dini. Katika riwaya ya *Paradiso* mwandishi ameonyesha kuwa ingawa watu wengi wameikumbatia dini ya kikristo dini hii haina nguvu juu ya tamaduni za kijadi. Watu wanapoingia katika dini huwa hawaachi tamaduni zao ambazo zinaenda kinyume na mafundisho ya Bibilia, kwa mfano mzee Mango anakuwa kiongozi wa kanisa lakini ana wake wengi. Desturi zinaonekana kufaulu kuliko imani za kidini. Sababu nyingine inayowafanya watu kuingia katika dini kama anavyosema mtaalamu wa Kiswisi Carl Gustar Jung(1875-1961)anazungumzia uto-ufahamu wa kijumla(pamoja na ule wa kibinafsi),hapa anamaanisha kuwa hata kama binadamu atayachukua mambo mageni ni vigumu kuyaacha yale ya kale, yaani hata akiingia dini ni vigumu kuacha utamaduni wake.

Waumini katika riwaya ya *paradiso* wanaendeleza mambo ya kale kwa mfano Lona kuenda kwa mganga ili amdhibiti mumewe ambaye ni askofu na Lona ni kasisi. Haya yanafanyika kwa sababu ya uto-ufahamu wa kijumla, waumini hawa hawana udhabiti kamilifu wa fikira zao kwa sababu wako katika himaya ya wanajamii wengine ambao hutenda mambo ya kishirikina hata bila kufahamu wanafanya vile. Mwandishi wa riwaya hii anaibeza dini ya Kikristo kama imani isiyo na mashiko,anakubaliana na mawazo ya Sigmond Freud(1865-1939)katika kitabu chake *The Future of an Illusion,*(1961:17)Sigmund alionelea kuwa watu huzua dini kwa sababu ya uoga,analinganisha wazo la kuwepo kwa Mungu na jinsi ambavyo watoto wadogo

huwaogopa wazazi hasa baba yao, ingawa wenyewe wanajua anaweza kuwakinga dhidi ya hatari yoyote,hivi ndivyo binadamu anavyozipa nguvu miungu Fulani. Miungu hawa humuondolea uoga unaoletwa na vitu kama kifo,magonjwa,na majanga mengine na pia hutoa jibu kwa mateso yote anayopata binadamu kama, umaskini na kadhalika. Freud anasema kuwa watu wanaogopa kifo sana na wanaweza kufanya lolote ili wajikinge nacho, hapa ndipo mwandishi wa riwaya ya *paradiso* anavyokubaliana na Freud kwa kuwa watu wengi katika makanisa haya wanatoka vitongojini na ni maskini. Riwaya inaeleza kuwa dini haiwezi kuwa suluhisho katika kila upungufu wa binadamu, na pia haiwezi kusuluhisha matatizo yote ya kimaisha, kwa hivyo dini ina nafasi duni sana katika maisha ya binadamu.

Kwa mujibu wa Mwita (2003)dini ni kigezo kimoja cha kuwagawanya watu duniani katika makundi ili kuwabagua. Katika mwongozo wake wa Walenisi, Mwita(2003)amenakili mahojiano kati yake na mwandishi wa riwaya ya Walenisi, alipomuuliza dini ina nafasi gani katika kuleta haki, usawa na maendeleo ya kijamii katika nchi,mwandishi alijibu "Dini ni sehemu moja ya utamaduni wa watu,lakini dini ambazo zilikuja na ubepari,zilikuja na dhuluma za kisiasa na kijanja, kutufanya sisi wajinga, sisemi kwamba dini si muhimu, dini ina misingi ya kutufundisha kuwa watu bora, kutufundisha nidhamu..."Mawazo ya Mwita na ya Mkangi yanatuangazia mtazamo wa wanajamii kuhusu dini na ndio msingi wa utafiti huu.

Naye Marx (1859) kuhusiana na dini alisema "Dini ni ishara ya kiumbe aliyekandamizwa moyo wa ulimwengu usiye na moyo,ni muhadarati wa wengi" Marx anaita dini kama muhadarati wa walio wengi kwa kuwa kulingana naye dini huwapumbaza na kuwalaza watu kwa kutumia imani yake katika mungu na matumaini ya hapo baadaye ya mbinguni.

Lenin naye anashikilia kwamba maovu ya dini yamo katika zile athari zake za kulevya zinazowatoa wanadamu kutoka kwa dunia halisi,anaendelea kusema kuwa dini kama pombe inamlevya mtu hivi kwamba mlevi hayumo katika hali ya uhalisi, dini inawanyima wafuasi wake maisha mema humu duniani kwa sababu wanaotea na kutumainia maisha mema huko mbinguni (Gehman1993:37-38). Nyaundi N. (2003:122)Anasema dini hueleza ni kwa nini matajiri wanafaa kuendelea kuwa matajiri na huwaliwaza maskini kwa kuwa kwa kuwa katika hali ile. Ukristo huhusisha utajiri na baraka za Mungu na umaskini hutazamwa hutazamwa kama laana, wakristo wanaelezwa kuwa maisha mema ni ahera na kwa hivyo hata kama wao ni maskini wasife moyo.

Kutokana na maelezo ya waandishi mbalimbali kuhusu mitazamo yao kuhusu dini,tunamwona mwandishi wa riwaya ya *Paradiso* akitaka kupitia kwa maandishi yake watu anawataka watu wafunue macho na kudadisi mambo ya dini na viongozi wake kwa undani sana,pia wasiyaamini yote wanayoambiwa na viongozi dhalimu wa kisiasa na kidini. Ameonyesha kuwa dini inaweza kuwa na manufaa pale ambapo inawasaidia wote kwa usawa bila kupendelea huyu na kumdhalilisha yule, dini ikieleweka vyema waumini wateisha maisha mema bila shida nyingi,tunapozungumzia dini katika muktadha huu tunamaanisha kufuata mafunzo ya Bibilia na

Kurani kwa ukamilifu bila kuvurugwa kwa manufaa ya kibinafsi. Tusisahau kuwa karibu dini zote ulimwenguni zilianzishwa na mwanamme na kwa sababu ya ubabedume,mwanamme alimtenga mwanamke kupitia kwa dini kwa kuleta dhana kuwa Mungu, Malaika na wafuasi wake wa karibu walikuwa wanaume kwa mfano katika Bibilia na Kurana, Mungu, Yesu, Muhamadi, Malaika na Mitume wote walikuwa wanaume. Katika dini ya Kiislamu kwa mfano kutowaruhusu wanawake waislamu

kuingia msikitini ilhali wana wao wadogo wanaingia vitendo kama hivi huwadhulumu wanawake. Kuna wale katika dini ya kikristo ambao hunukuu vifungu visivyowaruhusu wanawake kutawazwa kama viongozi wa makanisa. Dini imetumiwa kugawa jamii kuwili "wanyonge"wanawake na wenye nguvu "wanaume."

## 2.2 Athari za dini katika ndoa mbalimbali katika riwaya ya *Paradiso*

Riwaya ya *Paradiso* inabainisha masuala mbalimbali kuhusu dini na ndoa, wahusika wakuu wametuthihirishia uhusiano huu katika mtagusano wao wa kila siku. Bwana Mango ambaye ni babake Michael amekaa Mombasa kwa miaka Ishirini akifanya kazi bandarini. Mzee huyu ameoa wanawake watano, kama ilivyo desturi ya kwao Budalangi. Akiishi Mombasa na mke wake wa tano Zuhra, yeye alikuwa ameweka hawara akiitwa Sakina, wake wengine wa Mango waliishi Bunyala wakitegemea Uvuvi katika ziwa Victoria. Mwandishi anatubainishia kuwa kutokana na mauzo ya samaki wanawake hawa ndio waliolipa karo shuleni na kutimisha mahitaji mengine ya familia.

Kuwa hapana katika hao wake wane ambaye angetegemea au afikiri kuwa Mango angewatumia fulusi kufanyia haraja. Mchumo wote wa Mango uliishia katika Sakina hawara wake na kilichobakia kidogo kikawa cha mkewe mdogo, Zuhra. Pia Mango hakuenda nyumbani kwake huko Budalangi kwa urahisi labda tu apelekwe na mkasa kama wa matanga na au Krismasi, au masuala ya mashamba ambayo ingemlazimu kwa kuwa yeye ni mume. Haya yanabainisha dosari iliyokuwa katika ndoa ya mzee na masaibu waliopitia wake zake. Mwanzoni mwandishi anamwelezea Mango kama mtu aliyeishi bila dini maalum. Leo ni muislamu. Kesho ni mkristo. Kesho kutwa ni mtu wa dunia na mtondo na mtondogoo hajulikani.

Hata wakati Salma anapomuuliza kuhusu ugonjwa wa Michael na kuhoji apelekwe kwa waombezi Zuhra anamjibu kuwa baba mtu yaani Mango haamini mambo haya ya waombezi yaani dini. Mazungumzo haya kati ya Salma na Zuhra yanafichua tabia ya Mango ya kutompa mkewe uhuru wa kujiamulia mambo na amemuogofya Zuhra kwa kuwa amejua akimfanyia Mango kinyume anaweza kuachwa uoga huu wa unadhibitisha anachoelezea mwandishi Woolf.Kulingana na Woolf(1929)mwanamke hawezi kupata ukombozi wa aina yoyote kamahajakombolewa kiuchumi. Mango anatumia swala hili la kiuchumi kumdhibiti Zuhra.

Mango anaposhauriwa na mkewe Zuhra kuwa akubali tu Michael afanyiwe upasuaji yeye amekataa na hata kumwambia mkewe kuwa ushauri unaoweza kuuchukua tu ni wa mwanamume. Mango alichukizwa sana kusemezwa na mwanamke.

Alitaka yeye aseme na asikizwe tu dhana hii ni dhihirisha kuwa mzee Mango anaongozwa na imani ya ubabedume ya kuwadharau wanawake. Michael anapolazwa hospitalini alikuwa na Kibibilia chake cha Agano Jipya mfukoni, walichopewa shuleni mwao kongowea na mmishonari mmoja wa kizungu, Baba Joseck. Tunaambiwa, mwanzoni Michael alikisoma tu kama hadithi ya yesu. Lakini baada ya maradhi kumfumbata na michomo yake mikali alianza kuona bibilia kama kamba ya kumtoa katika mwina wa giza. Anapopata nafuu kidogo anakisoma kwa mazingatio na hata siku moja alikifunua kikafunuka katika sehemu ya mathayo 7:7 sehemu inayomwelekeza kuwa bisha na utafunguliwa. Omba na utapewa. Tafuta na utapata kila aombaye hupata. Maneno haya yalijenga ghera ya aina yake katika ubongo wa Michael.

Michael aliamini kwenye maneno ya yesu ambayo yalimpa matumaini, aliamini baba yake hakuwa mwingine bali yesu kristo kwa kuwa baba yake aliyemzaa alikuwa mithili ya kinyonga. Hana msimamo katika masuala ya itikadi kama haya. Michael alimheshimu lakini akaona yeye ataishi maisha yake tofauti maulana akimpa uwezo wa kuishi kila mja ana roho yake.

Michael pia anaota kuwa amemwona yesu mwana wa mungu akiwa ameubeba mzigo mkubwa mgongoni mwake inamuudhi kuwa mzigo huu wote ni dhambi za ulimwengu mzima lakini Yesu anakataa kuwa sio dhambi za ulimwengu mzima bali ni zake tu. Michael anaposikia vile anamwangukia yesu mguuni na kutubu ndoto hii huenda ni jazanda inayoashiria dhambi anazozibeba binadamu hata kuanzia umri mdogo. Apondi ambaye ni mke wa Mango wa kwanza (mamake Michael) alikuwa na wasiwasi kuhusu maradhi ya mwanawe kwa kuwa mwanawe huyo ndiye aliyekuwa tegemeo lake baada ya baba yake kumwonyesha dharau. Apondi anapofika Mombasa anashangazwa na mabuibui mengi waliojifunika wanawake haya mabuibui yanaletwa na utamaduni wa dini ya Kiislamu.

Ni dhahiri kuwa Mango hatekelezi majukumu yake. "Apondi anahoji kuwa mtu hana haya ya kipato chake kidogo hicho anajilimbikizia wanawake. Nyumbani sisi ameshindwa kutuangalia tunatamba na ukoko watoto kusoma hawawezi". Kupitia kwa matamshi ya Apondi mkewe Mango tunatafakari kuhusu nadharia yetu inayoangazia nafasi ya mwanamke katika jamii, kama anavyosema Wamitila (2002) kwamba, asasi za ndoa na dini hutumika kumkandamiza mwanamke. Mango anatumia asasi ya ndoa kuwadhalilisha wanawake, kwa kuwa ni dhuluma kuwaoa wake wengi, uzae watoto wengi na ushindwe kuwakimu kimaisha kama anavyofanya Mango.

Baada ya Michael kupata nafuu Mango anabadilika kuwa mungu ni mkubwa na kujiunga na kanisa la Pentecostal Assemblies of God siku nyingi Mango alikuwa ameona bibilia kama porojo la wayahudi. Lakini baada ya kitendawili cha maradhi ya mwanawe kuteguliwa na huyo mungu aliyekuwa akimkana Mango sasa alimwamini. Mango alishukuru kanisa la Pentecoastal Assemblies la Mishomoroni kwa kuwa mwanawe alikuwa Buheri wa Afya, Mango sasa alikuwa muumini, kule kanisani Mango alikuwa na tatizo moja, wakuu wa kanisa walimpa matakwa ya mwenyezi Mungu.

i. Kwanza asioe zaidi ya mke mmoja
ii. Asiweke kimada
iii. Asishiriki ulevi

Masharti haya yalimuudhi Mango na kumfanya aanza kudadisi kuwa; waislamu huoa wake zaidi ya mmoja, Daudi katika Bibilia Pia alikuwa na wake wengi, na akashangaa kuwa akiwataliki hawa wake wangeenda wapi?

Hili ndilo swala tunalolishughilikia kuwa masharti ya dini huathiri ndoa? Mango aliridhika na maelezo kuhusu injili lakini akaamua, kuwa atafanya atakavyo, kwa kuwa lililokuwa muhimu ni kuabudu huu ni unafiki ambao Mango anaingiza kanisani.

Michael alisumbuliwa, na jambo moja nalo ni kwamba, alitaka afanye jambo la kumuonyesha hewala Mungu kwa kumpa siku za kuishi.akaona atakuwa mwinjilisti liwe liwalo, ile mbegu ya kuwa mhubiri ilimea ndani ya Michael kila siku ikawa inanawiri katika nafsi yake, Michael alitaka asane watu kama alivyosana mbao.

Mango naye alifanywa mzee wa kanisa pale Mishomoroni. Hii kazi alipewa kwa ajili alijitolea sana kwa kazi ya kanisa na pia alimtolea Mungu zaka na sadaka, manung'uniko

si haba yalitolewa na waumini kuhusu uongozi aliopewa Mango, kinyume na mafunzo ya dini Mkristo anatakiwa awe na mke mmoja Mango ambaye ana wake watano anapewa uongozi kanisani. Watu walihoji kwamba Mango;

1. Alikuwa na wake watano na wote hawa hakuna aliyeolewa naye kwa harusi
2. Alikuwa na mke muislamu aliyeitwa Zuhra.

Mango alisumbuliwa na wazo kuwa mkewe alikuwa muislamu na pia anakataa kuandamana naye anapoenda kanisani.Inabainika kutokana na malumbano ya Mango na Zuhra kuwa Mango alipomposa Zuhra alimdanganya babake Zuhra Abdulla omwangola kuwa angeslimu na kuitwa swalehe. Suala la dini linataka kusababisha mtafaruku katika ndoa ya mzee Mango kati ya ni nani aabudi wapi na vipi?

Kipitia kwa dini Lona ambaye ni mama wa kanisa anakutana na Joshua ambaye alikuwa hana mahali pa kuishi na kwa hivyo anamkaribisha kwake, kwa idhini ya mumewe ambaye anaitwa Mganga.

Baada ya Joshua kukaa pale miaka kumi inabainika wazi kuwa Joshua alikuwa mume mwenza Mganga, Mganga hakujua lolote haya yalipoingia masikioni mwa waumini hawakuamini hapo ndipo Mganga alipoufahamu msemo usemao mgeni kumkaribisha kumbe ni kijitongea. dini inatibua ndoa ya mganga na Lona: Joshua asingeingia katika uhusiano huu ambao ulikuwa shwari mwanzoni haungevunjika, athari ya dini katika ndoa hii imejitokeza wazi. Joshua alipandishwa cheo katika kanisa la new Jerusalem na kuwa Askofu Mkuu licha ya yale aliyoyatenda katika ndoa ya Lona na Mganga.

Baada ya muda wazazi wake Michael walianza kumshinikiza aoe. Michael alikumbuka alipokuwa pandya Hospital maradhi yalipomshika kwa kucha kali alifanya suhulu na

Mungu. Kuwa akimponya hataoa na kuwa na familia. Alitaka kuwa kama Yesu Kristo ambaye hakuwa na mke. Hili ndilo suala tunaloliangazia kuwa kwa kiasi Fulani dini huathiri ndoa katika jamii kwa kuwa wale wanaoshikilia dini wakati mwingine hukataa kuoa kama anavyoazimia Michael.

Musa ambaye ni mumewe Rose aliingia katika uhusiano wa mapenzi na Salome. Musa alikuwa Askofu na anatumia cheo chake cha dini vibaya kwa kufanya mapenzi na mkewe Kyalo Muasya. Uhusiano huu wa Musa na mke wa mwenziwe una athari gani katika ndoa hii? Dini ndiyo iliyowakutanisha wawili hawa kwa kuwa Salome alikuwa mwanakwaya na mpambaji wa kanisa na Musa akawa Askofu.

Hizi ndizo athari za dini katika ndoa. Kyalo aliporudi usiku wa manane baada ya safari ya matanga kutibuka anamfumania mkewe Salome na askofu Musa kitandani Mwake. Mchungaji Musa Bosire ameingilia ndoa ya mwenziwe hadi chumba cha kulala inabainika wazi kuwa penzi la Kyalo na Salome lilikuwa la hali ya juu lakini Mchungaji huyu ndiye anayeingiza dosari. Kwa kuwa hata hospitalini Salome anapomuomba Kyalo Msamaha Kyalo ananena kuwa hata msamehe kwa sababu alimsamehe usiku ule ule. Salome anakiri kuwa aliingizwa mtegoni na Askofu Musa kwa ajili ya mtoto (alitaka apate mtoto) na hata Salome anavyomshinikiza Kyalo Kuoa mke wa pili ili aendeleze kisasi chake Kyalo anakataa na kusema alioa ili apate mshirika. Kupitia kwa ushauri huu wa Salome kwa mumewe Kyalo kuwa aoe ili apate watoto, inajitokeza wazi kuwa utamaduni umemuathiri mwanamke kwa kiasi kikubwa kwamba,amejidharau hadi ndoa yao isipopata watoto anajiona kama yeye ndio ana dosari.

Kiongozi huyu wa dini Askofu Musa anautumia udhaifu wa Salome wa kutopata mtoto na kumnasa katika mapenzi naye bila kujali ni mke wa mtu. Kyalo alimwona kasisi Musa kama afriti laghai aliyepoteza kondoo alopewa kuwatunza na kuwaangalia.

Inajitokeza kuwa Askofu Musa hakuwa tu akimhadaa na kumchezea mkewe Kyalo bali wanawake wengine karibu watano wote ni wake wa watu na mmoja ni binti ya mtu katika shule ya Alliance. Kyalo alishangaa kama huwezi kumwamini mhubiri utamwamini nani? kama kanisa siyo mahali pa salama watu watakimbilia wapi? Athari ya dini inajipuka wazi katika ndoa.

Bwana Mango amelazwa hospitalini kwa kupewa sumu kanisani, kisa na maana ni kupigania uongozi wa kanisa na sadaka, pia inabainika kuwa mwezi uliopita wanaume kumi walitiliwa sumu katika mchuzi wa nyama na wakafa wote, mama Julia amefanyiwa dawa akashikwa na wazimu haya yote yanafanywa katika makanisa ambayo yanatarajiwa yawe kielelezo bora katika jamii. Musa naye anapopona anaamua kuyaasi tena mambo ya kanisa na kuingia katika biashara ya mitumba na matatu. Musa aliamua pia kumkataza mkewe kwenda kanisani kwa kuwa aliaibika kurudi kanisani.

Baada ya Mganga kuachana na Lona yeye aliwachukia wanawake wote na kuamua kuishi maisha ya upweke. Katika mambo aliyopiga marufuku maishani yalikuwa mambo ya dini aliona dini kama ulaghai na ujambazi.japo mamake alimhimiza aoe hakuona haja, mganga hakutaka shughuli yoyote na mwanamke na hata wahudumu wake walikuwa wanaume,aliwaonya wasilete wanawake katika mji ule na pia aliichukia dini (Hivi vyote alivichukulia kama chanzo cha masaibu ya maisha yake). Joshua na Lona ni viongozi wa dini lakini wanataka kulazimisha ndoa kati ya Michael na Nice bila hiari yao. Nice anaposhinikizwa kuwa aolewe kwa Michael, kwa kuwa Michael ni mtu wa dini yeye

anakana kuwa yeye (Nice) si mtu wa dini kwa hivyo ndoa kati yao haifai. (Athari ya dini inafanya Nice asipende kuwa kwa ndoa na Michael).

Katika mazungumzo kati ya Joshua na Lona kuhusu kauli ya Musa kuwahusu alipokuwa wazimu mjini inazua athari nyingine ya dini kuhusu mwanamke katika ndoa kama anavyosema kasisi Joshua kuwa " Wajua nyinyi wanawake sijui akili zenu ni ndogo vipi? Si ajabu Mungu akasema ni viumbe duni nyinyi?" Hii kauli kutoka kwa kasisi anayetakiwa kuwahubiria watu kuhusu masuala ya ndoa ni hatari mno. Nice aliporudi nyumbani, baada ya miezi minne, Nice alikuwa amekaa bila kuwatembelea, Askofu Joshua alimshambulia na maswali chungu mzima. Lakini kwa ujeuri Nice alimpasulia mbarika kuwa yeye alikuwa amerudi kumwona mamake na hakutaka kubughudhiwa na mtu ambaye hakuwa babake. Joshua ambaye alikuwa ameipenda familia yake na dini anaingiwa na kiwewe baada ya utambuzi huu kumbuka, Joshua alimpokanya Lona kutoka kwa kinywa cha mume mwingine kwa kuzingizia suala la dini na sasa kitumbwa chake kimeingia mchanga.

Anapokuwa katika msitu wa Langata, Joshua anaanza kuwaza "Ni kweli nimemhadaa mungu kwa siku nyingi. Nilikuwa siku zote hizo nafikiri nawajengea Nice na Judy Maisha ya Baadaye kwa kuwawekea viekezaji vya uchumi..." Joshua akiwa katika msitu wa Langata anaingiwa katika mawazo kuhusu kile ambacho angekifanya ili amjue babake Nice ambaye aliishi akidhani ni mwanawe anashuku hata kama Judy pia ni mwanawe anaazimia kuanguka miguuni mwa mwenyezi mungu pasi na ujanja na unafiki bali ukweli kauli hii inaturudisha katika wazo letu kuwa viongozi wa dini ni wajanja na suala la dini linapotumiwa vibaya linaweza kusababisha madhara makubwa katika ndoa.

Joshua na mkewe Lona wameishi katika kudanganyana kwa muda huu wote. Mawazo haya ya Joshua yanaturudisha katika mada yetu kuwa dini zinaathari kuu katika ndoa yasipotumiwa vizuri. Joshua anayakumbuka mawazo ya mfalme Suleiman kwamba dunia si chochote? Kumbe pesa, wanawake, uongozi si chochote? Aliona muhimu ni kuzingatia maadili ya kristo. Hapa ndipo tunapotambua kuwa dini ya Joshua na Lona haikuwa ya kweli hapo mwanzoni ndiposa inasababisha balaa katika ndoa yao.

Kitumbua kinapoingia katika ndoa ya Joshua na Lona, Lona anaamua kuomba usaidizi kutoka kwa rafiki yake Adema, maelezo yanayotolewa kuhusu Adema ni kuwa alikuwa katika Afrikan devine Church baada ya kutoka katika legio Maria. Huyu ni kiongozi wa akina mama katika kanisa ya African devine Church, Lakini kinachoshangaza ni ushauri anaompa mke wa Askofu Joshua, Lona. Anampeleka kwa mwanamke mganga kule kawangware huku wamebeba chupi na nywele za Joshua eti "Kumkomaza" kama "alivyokomazwa" bwanake Adema. Hawa wanawake wawili ni viongozi katika dini zao, ndio wanaotakiwa hata kuwashauri wanawake wengine mizozo inapoibuka katika ndoa za waumini wengine lakini wanayoyafanya ni mambo ya kichawi hili linaonyesha kuwa dini ina athari nyingi mbaya katika ndoa.

Tunapokumbana na Michael tunaona athari za dini zikitaka kumzuia kuoa. Alihisi kuwa angemtumikia bwana vyema kama hangeoa. Mwandishi katika (uk 113) anatupa madhumuni mbalimbali ya watu kwenda makanisani, kuwa kunao waliofanya ya shari pia waliofanya ya shwari kunao ambao makanisa yalikuwa kama vyama vya ushirika kwamba mtu akifa aweza kufanyiwa mchango wa kusafirishwa nyumbani. Kulikuwa na makanisa ambapo watu walikwenda kutupa wakati kwa sababu ya uvunjafu. Mengine yalikuwa mahali pa kwenda kama mazoea bila kuwepo na sababu maalum. Mahubiri

kwa watu kama hao yalikuwa kelele ambazo hazikuwashtua wale ambao masikio yao yalikataa kusikiliza, haya ndiyo makanisa na dini ambazo mada hii inazungumzia ambazo zina athari kubwa katika ndoa kwa kutoa mwelekeo usiofaa kwa waumini.

Michael mwishowe aliamua kumuoa Lidia kwa harusi ya kidini iliyofana sana. Michael anapokuwa katika mawazo kuhusu vile hamasa za dunia zinaathiri dini anakabiliwa na mkewe Lydia anayemwambia katika (uk 125) kuwa " haya mambo yako ya dini huwa na kwambia yatakutia wazimu siku moja" hili linaturudisha katika mada yetu kwa kuangazia athari ya dini katika ndoa.

Joshua anapoambiwa kadhia za Nice kule ng'ambo anahuzunika, lakini wazo linamjia kuwa vitendo vya mzazi huwa mfano mwema kwa wana, yeye Joshua hakuwa mwaminifu wala Lona hakuwa mwaminifu. Uaminifu wao ulikuwa midomoni tu. Kama Askofu na mkewe wanaweza jitambua kuwa wanafiki, swali ni kuwa ni nani anayeweza kuongoza kondoo (waumini) hili ndilo suala tunaloliangazia katika riwaya hii yaani athari za dini katika ndoa, kwa kuwa dini imeongozwa na wanafiki wasioweza kuwaelekeza waumini katika masuala ya kindoa. Tunaelezwa Joshua na Lona walikuwa wamemchukia sana mshiriki mwenzao na Binamuye Joshua ambaye aliitwa Boribori, kisa na maana kikiwa Lona alienda kwa Boribori akitaka mahaba naye ati kwa kuwa Joshua alikuwa hampendi tena, Boribori akamkatalia Lona kwa macho makavu, Boribori hakuona ni Vipi angelala na mke wa Askofu tena rafiki na Binamu yake. Mbeko na maadili yake hayakumkubalia kufanya hivyo. Joshua hakuona haya maovu kwa kuwa alikuwa amefungiwa na Lona, huyu mke wa Askofu ndiye aliyesababisha chuki kati ya Joshua na Binamu yake kwa kusema uongo kuhusu Boribori; alimdanganya Joshua kuwa Boribori alitaka kumnajisi.

Zuhra ambaye ni muislamu kwa mara nyingi hakuridhika na matendo ya wakristo wengi japo walisema wameokoka matendo yao yaliwasaliti. Baada ya Lydia kujifungua ndoa yao na Michael inaingia dosari. Michael alianza kumpenda Patricia na hata kujiuliza,kwa nini alimwoa Lydia. Ubaridi ulimwingia Michael na hata mambo aliyokuwa akimfanyia mkewe yalibadilika, kama kumletea zawadi, kuandamana naye safarini na hata kuonyesha kuguswa na matatizo ya Lydia, haya yote Michael hakuyatekeleza. Naye Patricia alibadilisha maisha yake mwanzoni aliuchukua wokovu kidogo tu,lakini baadaye aliuchukua wokovu wake kwa moyo wake wote. Alianza kusema kwa ndimi na hata kusoma Bibilia kila mara na majarida ya kidini. Baada ya muda mwingi Lydia alikataa kuamini kulikuwa na jambo lolote baina ya mume wake na Patricia maana hawa wawili ndio watu aliowaamini, Patricia alikuwa mwandani wake, Lydia hakujua sasa Michael alimtembelea Patricia kuliko alivyofikiria, kama kiongozi wa dini Michael alijiwa na Patricia ili ampe ushauri. Afisini mwake pale Bethany, Patricia alitaka ushauri kwa ajili ya upweke wake, hakujua afanye nini, Walizungumza pale afisini, Michael mwili unapomzidi anamkumbatia Patricia ambaye alikuwa akilia na kumpiga kisi, mapenzi yao yanaanzia pale Michael anamzoea Patricia na hata hajali kuwa yeye ni Mtumishi, Michael sasa kama baba yake alikuwa na dunia mbili kwanza,dunia ya imani kwa bwana na mapenzi na Patricia. Mwendo wa Michael ulianza kubadilika wengi, Salome akiwamo hawakuamini kuwa Michael angeangukiwa na mtego huo, Salome alikumbuka yaliompata na ni Michael aliyemshauri jinsi ya kumrejelea Bwana Yesu. Michael alikuwa akihubiri dhidi ya mahusiano kama haya yaliyomtenga mtu na muumba wake. Na sasa yeye ndiye aliyekuwa ameingia mtegoni, Salome alishangaa

ni kwa nini dunia imebadilika hivyo. Michael ambaye alikuwa mhubiri mashuhuri sasa amenaswa katika utando wa mapenzi ambao unaathiri ndoa yake pakubwa. Ameingia katika bwawa na tope, bwawa la maangamizi na bwawa la kishetani.Mama mmoja Aoko alidai kuwa aliwaona Michael na Patricia katika hoteli moja ya Sunset kule Kisumu, uhusiano huu wa Michael na Patricia unalipiga kanisa dafrao hadi likavunjika vipande viwili. Lydia kwa upande wake alikuwa kasha shikwa na mawazo mengi, alikuwa ameanza kuwa mnyonge, Lydia hakuamini kuwa Patricia ndiye aliyemzunguka nyuma. Lydia alishangazwa na tabia ya Michael ya Kutojali afikapo nyumbani anajali tu afikapo kanisani wakati wa kuhubiri na kudai ni shahidi wa Bwana Yesu. Hata alipomwambia Michael angeenda Mombasa Michael anaonyesha kutoshughulika pia hamsindikizi anapoondoka, kiongozi wa dini anayetegemewa kuwaongoza wafuasi wake sasa ameingiza doa katika ndoa yake kinyume na mahubiri ya Bibilia anayoyatoa, hapa ndipo tunapopiga tarubini kuhusu athari ya dini katika ndoa hata za wahubiri. Patricia ambaye pia alikuwa ameokoka na Michael ambaye ni kasisi wanaingia katika uhusiano ambao unayumbisha ndoa ya Michael na Lydia.

Lydia anapoenda kutafuta ushauri kwa mamake kule Mombasa, wawili hawa wanaamua kwenda kwa Mango ambaye pia ni kasisi ili awasaidie kurekebisha mambo katika ndoa ya Michael na Lydia, lakini Mango anaonekana kuegemea upande wa Michael na hata kumshauri Lydia kwa kutumia kifungu cha Bibilia kuwa asiyasikilize ya watu kwa kuwa kitabu cha mithali nne kinasema mwanamke mjinga huvunja nyumba yake kwa mikono yake. Kinyume na matarajio yake kuwa viongozi wa dini wanatarajiwa kusuluhisha mizozo ya ndoa Mango anaendelea hata kuongeza mzozo.

Hata wanapotoka kwa Mango wakiwa wamekasirika Zuhra anajaribu kuwazuia lakini Mango anasema kwa kiburi kuwa "waache waende" tabia ya Mango inamshangaza Lydia na mamake ambaye anamuona Mango kama mzazi na kasisi mwenye kuhubiri umoja,amani na upendo. Ni dhahiri kuwa unafiki katika dini ndio unaosababisha mizozo katika ndoa kwa kuwa wahubiri hawafanyi wanavyohubiri na waumini pia wamefuata mkondo huo.

Ni kweli kuwa Michael alikuwa amemranda babake. Ingawa Lydia alikuwa karibu akate tamaa lakini alipata walimu waliomtia chuoni na kumfunza, alinolewa na sasa alikuwa keshapata makali. Mwanzoni alikuwa ameamua angepahama pale walipoishi yeye na mwanawe. Sasa aliamua kukaa hata kama ni kufa atakufia pale. Alisema, kwani mwanamke atakimbizwa hadi lini na wa kumkimbiza si mwanamume bali mwanamke mwenzake.Kitumbua cha ndoa ya Lydia kinaendelea kuingia mchanga hasa pale anapoarifiwa kuwa Patricia alikuwa mjamzito na mimba ilikuwa ya Michael. Hili linamsumbua sana Lydia akili na hata anaomba ruhusa kutoka kazini kwa kuwa hangeweza kufunza.

Tunaambiwa kuwa kutwa nzima Michael alikuwa akimshauri mtu na mkewe jinsi ya kuishi kwa amani. Hata yeye mwenye alijihisi kuwa hakufaa kushauri kuhusu matatizo kama yale. Ilibidi ajilazimishe na ashauri hivyo hivyo.Michael anaanza kujiuliza kuwa "kwani ni mimi peke yangu? Wahubiri wanafanya wangapi kwa jina la Yesu na wanazidi kuendelea?"

Ndio wenye magari bora siku hizi ndio wenye nyumba za bei. Ndio wanaosomesha katika skuli za ghali na ndio wanaojilimbikizia pesa benki. Ni kinaya kuwa haya maneno yanatolewa na mtu ambaye anategemewa atoe ushauri katika ndoa za wengi,

hili linatubainishia kuwa hawa viongozi wa dini badala ya kuleta amani katika ndoa ndio wanaoleta mizozo hata zaidi.

Baada ya kushindwa kukumbana na matatizo ya mumewe, Lydia aliona ni vyema anywe pombe, anaporudi nyumbani anazua ugomvi na hata kumsaba Michael makofi kadha, wanaanza kupigana na hata Michael anapomrusha chini anafikiri amemuua mkewe. Vilio vya wanawe vinawaleta majirani ambao wanasaidiana kumpeleka Lydia hospitalini.

Tunaambiwa baada ya mtafaruku kuanza, Lydia alikuwa akilala katika chumba chake peke yake. Lydia amelazwa hospitalini, polisi wanamchukua Michael ili wamhoji,. Pia yeye na mkewe hawaonani jicho kwa jicho haya yote ni madhara dini inayosababishia ndoa katika jamii. Inabainika kuwa Lydia amevunjika ubavu mmoja na pia amepata majeraha ya kichwa. Mambo haya yote yanadhibitisha kauli yetu kuwa dini inaathari kubwa katika ndoa kwa sababu ya unafiki wa viongozi wa dini,na wanaoathika sana katika muungano huu wa ndoa ni akina mama.

### 2.3 Matatizo ya wanawake katika ndoa yanavyosawiriwa katika riwaya ya *Paradiso*

Woolf (1929) analipa uzito swala la uchumi kwa ukombozi wa mwanamke. Anadai kuwa mwanamke hawezi kupata ukombozi wa aina yoyote kama hajakombolewa kiuchumi. Katika jamii nyingi ulimwenguni, nyenzo zote za kuzalisha mali zinatawaliwa na wanaume huku wanawake wakiwa wategemezi na watumishi wa wanaume. Hali hii huwakumba wanaume kwa sababu tangu zamani wanawake wamenyimwa nafasi ya kujiendeleza kiuchumi,kwa kawaida maisha ya binadamu hutegemea uchumi, hali ya uchumi ikiwa mbaya maisha ya binadamu yanakuwa mabaya. Walio na uwezo wa kiuchumi wanatumia nguvu zao za kiuchumi kwa kuwatawala na kuwanyanyasa wengine

kama anavyofanya Mango amewaoa wake wengi na kwa kuwa wake hawa hawana uwezo kiuchumi inawabiti wavumilie katika ndoa isiyokuwa na lolote zuri.

Wooolf(1929)anapendekeza kuwa ikiwa mwanamke atapata uhuru wa kiuchumi basi ataepuka manyanyaso na dhuluma kama wanazofanyiwa wakeze Mango, Apondi anahoji kuwa "Mtu hana haya ya kipato chake kidogo anajilimbikizia wanawake. Nyumbani ameshindwa kutuangalia tunatamba sisi na ukoko.Muhogo ni huo huo asubui na jioni. Watoto kusoma hawawezi" hili linadhirisha kuwa Mango anawadhulumu wanawake hawa kwa kuwa hawana uwezo kiuchumi wanalazimika kuvumilia. Waasisi wa ufeministi wakiwahimiza wanawake watafute njia za kuwawezesha wajitegemee kiuchumi, mbinu wanazopendekeza ni pamoja na kujiunga katika vikundi mbalimbali vya akina mama ili waweze kusaidiana na kupeana nguvu za kiuchumi.

Mbatiah(1994)mila na desturi za waswahili zinachangia sana katika kumweka mwanamke katika nafasi ya chini katika jamii,wanawake wengi huwa wamefungwa katika tamaduni ambazo kwa kiwango kikubwa huwadhulumu. Anayosema Mbatia yanajitokeza katika riwaya hii "Apondi alishangazwa na mabuibui mengi yaliyokuwa katika mji ule. Wanawake wengine walijifunika ninja kabisa nyuso zisionekane ila macho tu ya kuona njia." Kwa maoni yetu huu ni unyanyasaji wa mwanamke kupitia kwa mila na utamaduni wa waswahili kama anavyosema Mbatiah.

Osoro (2002) Anasema kuwa miongoni mwa vipengele vinavyomdhalilisha mwanamke ni pamoja na wasia.Tuki (1981:317) wanafafanua wasia kuwa,ni maagizo ya mtu kwa mtu au watu wake ambayo anataka yatimizwe iwapo atakufa au kuondoka. Tunampata Mwanakupona alipokuwa mgonjwa katika utenzi wa mwanakupona anamuusia bintiye kuhusu vile anapaswa kumtunza mume. Utenzi huu wa Mwanakupona unamwathiri Bi

Mosi katika Kiza Katika Nuru (1988:47-48) kwa mfano, Bi Mosi alipenda kuimba wimbo huu wa Mwanakupona kwa mwanawe Bi Kudura.

Bi Mosi alipenda kuimba:

Keti naye kwa adabu
Usimtie ghadhabu
Akinena simjibu
Itahidi kunyamaa
Kilala sii kukuse
Umwegeme umpapase
Na upepo asikose
Bi Mtu wa kumpepea

Wimbo huu wa Mosi bila shaka umemwathiri pakubwa Bi Kudura kwa kuwa baada yake kuondoka Bi Kudura aliushikilia wasia huu kama hirizi na hata kuhimili mateso katika ndoa ili atimize wasia wa mamake.

Mbatiah (1994) anasema kuwa dini imetumiwa na wanaume ili kumdunisha mwanamke na kumdhalilisha katika maisha ya ndoa. Hivyo ndivyo watafiti wengi walivyohisi katika utenzi wa mwanakupona, wengi wanaona kuwa mwanakupona alitumimia mafunzo ya dini ya Kiislamu ili kuhalalisha yote aliyoyasema. Tunachosisitiza katika utafiti huu wetu ni kuwa dini inapotumiwa vibaya ndipo inavyoathiri ndoa na kumdhalilisha mwanamke.hili linajitokeza kwa wasia huu wa mwanakupona kwa kuwa ameyatumia mafunzo ya dini ya kiislamu visivyo.kwa sababu dini ya kiislamu haihalalisha udunishaji wa mwanamke.

Wollstonecraft (1972) anasema kuwa elimu ndiyo msingi wa kila kitu maishani na kukosa elimu ni kukosa kitu cha thamana kubwa maishani. Elimu ndiyo inayoweza kumfanya mtu ajielewe, aielewe jamii na kupata kazi nzuri. Jamii kwa muda mrefu,

imemnyima mwanamke elimu bora, kazi bora na haki maishani. Wanawake katika riwaya hii ya paradiso wamenyimwa elimu bora na hii ndiyo chanzo cha masaibu ya wakeze Mango ambao hawajasoma na kwa hivyo kama anavyosema Wollstonecraft hawajielewi, hawaelewi jamii na hawawezi kupata kazi nzuri.

Mbatiah (1994) naye anaendeleza kuwa,pamoja na dini na utamaduni ukosefu wa elimu unamfanya mwanamke kuwa mbumbumbu katika jamii, kama alivyo Apondi na wenzake katika riwaya hii. Mbatiah anaendelea kusema kuwa, ukosefu huu wa elimu na kazi bora ndio husababisha matatizo ya kiuchumi na kumfanya mwanamke kama kiumbe anayetegemea mwanamme kwa mahitaji yake muhimu hali hii humfanya mwanamke kuwa mtumwa wa mwanamume. Anayosema Mbatiah yanadhihirika katika riwaya hii ya paradiso kwa kuwa wakeze Mango wana matatizo mengi ya kiuchumi na haya matatizo ndiyo yanayowafanya wamtegemee Mango na kuwa kama watumwa kwake.

Lydia anapojifungua mwanawe wa kwanza ndoa yao na Michael inaingia dosari, Michael anaanza kumdharau mkewe.na hata Lydia anapoenda kumlalamikia mamake, hawa wawili wanaamua kwenda kupata nasaha kutoka kwa babake Michael. Mango anakataa hata kuungama na malalamishi ya Lydia, maoni haya ya mzee Mango kwa Lydia kwamba, mwanamke mjinga huvunja nyumba yake kwa mikono yake, yanaturudisha katika maoni ya wafeministi kuwa makosa yakitokea katika ndoa mwanamke ndiye anayelaumiwa kwa sababu amesawiriwa kama kiumbe hasi, kama anavyosema Gaskof (1971) kuwa kwa muda mrefu watu wamevitumia vifungu Fulani Fulani vya bibilia ili kumdhulumu na kumnyanyasa mwanamke huku wakimuonyesha mwanamume kama binadamu kielelezo Mango anajitokeza kama mmojawapo wa watu hawa kwa kuwa anatumia kifungu cha bibilia kumulaumu Lydia kama mwenye makosa

hata kabla ya kupata ukweli wa mambo. Lydia anapomkabili Michael baada ya kunywa pombe anarushwa chini na hata kuvunjika mbavu, kama anavyosema Katola (2006) mwanamke katika ndoa anapitia udhalimu mwingi kama, kutusiwa, kupigwa na kunyimwa haki, Lydia anakuwa mhasiriwa wa haya hata haki za kimsingi ananyimwa na mumewe kwa kuwa tunaambiwa "...aliingia katika chumba chake ambamo alikuwa akilala peke yake siku hizi tangu kuingia mtafaruku baina yake na mkewe..." Mwanamke mwingine ambaye anakumbwa na matatizo chungu nzima ni Patricia, amebeba mzigo wa watoto wake wawili aliowapata nje ya ndoa bila kusaidiwa na wanaume, babake mtoto wa kwanza alikuwa mwalimu na alipopata mimba, mwalimu huyu alimtisha kwa kisu, huyu wa pili pia alihadaiwa na kijana mwingine hadi akapata mimba Patricia ametorokwa na marafiki zake na anakumbwa na mateso chungu nzima, pia amedungwa mimba nyingine na Michael. Mizigo hii yote inayosababishwa na mwanamume mwanamke ndiye hubeba kama anavyofanya Patricia na mamake.

**2.4 Hitimisho**

Katika sura ya pili tumeitanguliza sura hii kwa kutathmini mtazamo wa dini ya Kikristo kuhusu ndoa, pia tumehakiki athari za dini ya Kikristo katika ndoa mbalimbali katika riwaya ya *Paradiso*, na mwisho tumechunguza matatizo ya wanawake katika riwaya ya *Paradiso*.

# SURA YA TATU

## 3.0 Utangulizi

Sura ya tatu inaangazia mtazamo wa dini ya Kiislamu kuhusu ndoa, pia athari za dini hii katika ndoa na matatizo anayopitia mwanamke katika jamii ya Uislamu ndoa imechukuliwa kama mojawapo wa taasisi muhimu. Uislamu ni njia ya maisha ya wale wanaoamini mafundisho ya kurani,hadithi pamoja na uzingativu wa dini ya Kiislamu (Momanyi.1998). Katika sura hii twatarajiwa kutathmini jinsi ambavyo maisha ya mwanamke yanavyosawiriwa katika ndoa. Tutafanya hivi kwa kurejelea kazi ya S.A.Mohamed ya *Utengano* kwa kuwa riwaya hii iliandikwa kuhusu wanawake tunadhani kwamba riwaya hii itakuwa kioo cha kumulika maisha ya wanawake hao.Inabainika kuwa kiuchumi wanawake walilipwa mishahara midogo kuliko wanaume, kwa sababu ya ubaguzi huu, kazi za wanawake zilidharauliwa hasa za nyumbani kwa sababu hazikuleta ujira wowote. Kama Engels (1844)anavyosisitiza kudharauliwa kwa kazi za binadamu huambatana na kudharauliwa kwa hadhi yake, kutokana na dhana hii tunaona kuwa kipimo cha umuhimu wa binadamu ni faida ya kazi zake. Kwa hivyo kudharauliwa kwa kazi za wanawake kulileta kudharauliwa kwao kisiasa na kijamii.

Dini ni mojawapo ya taasisi ambayo imemtukuza mwanamume na kumdunisha mwanamke, msimamo wa dini nyingi kuhusu nafasi ya mwanamke umesaidia sana kuwachochea wanaume kuwa wazembe zaidi. Dini inawathibitishia kwamba Mungu alipomuumba mwanamke alimuumba kwa minajili ya kumsaidia mwanamume katika harakati za kupambana na matatizo ya kidunia kama anavyosema Lugano(1989).

Dini ya kiislamu imechanganyishwa na wingi wa utamaduni wa waswahili kwa hivyo ni vyema kuangalia utamaduni huu. Kulingana na Fredrick Engels (1975 : 128)

tofauti kati ya mwanamume na mwanamke zilitokana na ugawaji wa majukumu tangu enzi za giza, ugawaji huu ulileta hali ya utabaka katika jamii hali ambayo imeendelezwa hadi sasa. Katika hali ya uana umilikaji wa mali ulimwendea mwanamume ukiwamo pia uakifishaji wa mali! Kutokana na jukumu lake la kuzaa, mwanamke aliishia kujitambulisha na majukumu ya uzazi na malezi majukumu tofauti na yale ya mwanamume, ingawa mwanamke alifaidika katika starehe hii ya umilikaji wa mali ya mwanaume, hakuwa na nguvu ya kutoa maamuzi kuhusu mali hiyo ambayo haikuwa yake. Kutokana na tofauti hizi za kizazi nafasi ya mwanamke iliendelea kuwa nyuma tangu kale, na jamii ikafunzwa kuamini kuwa mahali pa mwanamke ni nyumbani na malezi ya watoto (Figer :1978)

### 3.1Athari za dini ya Kiislamu katika ndoa

Tumechagua riwaya hii kwa sababu ni moja ya baadhi ya riwaya ambazo zimezungumzia kwa undani sana jinsi hali ya mwanamke ilivyoathiriwa na dini. Mwandishi huyu amejishughulisha na hali ya mwanamke katika jamii kuliko waandishi wengi na ndivyo tukaona kuwa angetufaa zaidi katika kuangalia jinsi maisha ya ndoa yanavyomdhalilisha mwanamke (ndoa pamoja na dini). Wahusika wengi katika riwaya ya Utengano na kama mwandishi mwenyewe anavyosisitiza, dhamira yake ni kutetea maslahi ya walio wengi kwa hivyo kwa kuwatumia wahusika wanawake mwandishi anaonyesha umuhimu wa wahusika hawa katika jamii na vile dhuluma kwao zinaweza kusambaratisha jamii nzima. S.A.Mohamed ni mwandishi mashuhuri aliyejulikana sana, hasa kwa uandishi wa riwaya. Baadhi ya riwaya ambazo zimechapishwa ni *Asali Chungu, Utengano na Dunia Mti Mkavu*. Mbali na riwaya pia mwandishi ameandika mkusanyiko wa mashairi.

Riwaya ya Utengano kama jalada lake linavyoeleza ni riwaya ambayo inajaribu kuonyesha jinsi Maimuna, mwana wa nyumba kubwa alivyobadilika kulingana na mabadiliko katika mazingira yake. Mwandishi anajaribu kuonyesha kiini na matokeo ya mabadiliko haya. Tunapokutana na Maimuna kwa mara ya kwanza katika riwaya,tunamuona kama mtoto mwenye tabia nzuri ambaye anawatii na kuwapenda wazazi wake. Utiifu wake unajitokeza kwa kuwa yu radhi kusononeka na kuumia badala ya kuzivunja sheria za kinyama za babake, Bwana Maksuudi.

Sheria hizi zimemnyima Maimuna na mamake Bi Tamima uhuru wa kutoka nje. Tunaambiwa kuwa Maimuna aliruhusiwa kutoka nje mara chache sana na alipotoka, kila wakati aliandamana na mtu, isitoshe alipotoka alipelekwa na kurudishwa garini. Hayo ndiyo yaliyokuwa maisha ya Maimuna tangu utotoni na kwa sababu ya umri wake, aliyakubali bila pingamizi.

Hata hivyo ni lazima tufahamu kuwa, kukua kwa mwanadamu kimwili kunaambatana na kukua kwake kisaikolojia. Ukuaji huo unaambatana na mabadiliko katika hisia na fikra, basi si ajabu kuona Maimuna anaanza kuisi kuwa maisha yake si makamilifu, anatambua kuwa kufungiwa ndani kwake kwa muda huu wote kumemnyima haki pamoja na uhuru. Yeye na mamake hawana uhuru wa kutoka nje angalau kwa kubadilisha hewa. Kasoro inayoletwa na hali hii katika maisha huwa imeelezwa vizuri na mwana elimu jamii (White 1977).

> "Kuridhika kwa hisia ni kitu
> Ambacho cha chukuliwa kuwa
> Muhimu. Hali hii huletwa na
> Maingiliano ya mara kwa mara

Kati ya wanajamii na utafiti umedhibitisha

Kuwa,mbali na mahitaji muhimu ya chakula,

mavazi na malazi, watoto wanahitaji mambo

mengine kama mapenzi, michezo na mihimizo

katika juhudi za uvumbuzi." (Tafsiri yetu)

Kutokana na dondoo hili, tunaona kwamba Maksuudi babake Maimuna alikosea kumnyima uhuru kwa sababu jambo hili lilileta pengo na kasoro katika maisha yake. Mara nyingi Maimuna alilia kwa sababu ya kutengwa na dunia. Maksuudi alihakikisha kwamba mwanawe Maimuna na mkewe Bi Tamima hawakutoka nyumbani au kutembelewa bila ruhusa yake. Kama anavyosema Bi Tamima ...babako hataki tutoke nje ila kwa ruhusa yake na humu asiingie mtu

Ila kwa ruhusa yake"

Maksuudi bila shaka amepitwa na wakati, yeye anatakiwa atambue wakati wa kuwatawisha wanawake nyumbani haupo tena. Maimuna mwenyewe anatueleza kuwa babake, anamtenganisha na mazingira halisi ya wakati wake. Tendo hili linamuumiza na kumkandamiza,

"si kama haoni unyonge

si kama hadhikiki

anakonda na kudhikika

na linalomkondesha ni utawa

akikumbuka huona maonevu,

hasa akisoma na kusikia kwenye

redio jinsi wanawake wenziwe

wamepiga hatua katika maendeleo

ya nchi yao. "

Kutokana na nukuu hii tuna muona Maksuudi kama mhusika anayeongozwa na damaduni za waswahili ambazo ziliwadhalilisha wanawake kwa kuwatawisha.

Kurani tukufu ni msahafu unaobainisha wazi majukumu ya wanaume na wanawake, msahafu huu hauna maelezo yoyote yanayowakataza wanawake kushiriki katika nyadhifu za nje, nyadhifu za kisiasa au katika uongozi (Momanyi 1998, Ashgar 1985 : 100). Sheria ya dini ya kiislamu huwalinda wanawake dhidi ya maonevu ili kuhakikisha kwamba wanathaminiwa.

Waswahili wamezichukua mila na itikadi zao, na chini ya kivuli cha dini wamehalalisha ubwana na utwana, mbali na kuainisha majukumu ya mwanamke na mwanamume, kinachochukuliwa kama mtazamo wa waislamu kuhusu ndoa sio bali ni mtazamo wa waswahili kuhusu ndoa kwa sababu waswahili wameingiza tamaduni zao katika dini.

Katika jamii hii talaka ni jambo la dharura kutekelezwa hasa iwapo mke amedhihirisha utovu wa nidhamu ukiushi wowote unaopinga utovu wa jamii ulioko hauvumiliki kama inavyobainika katika riwaya ya Utengano Maksuudi kumpa talaka mkewe hata bila kufikiria kwa kina.Fasihi simulizi katika utanzu wa nyimbo za Waswahili pia zinasawiri jukumu la wazazi katika uchaguzi wa mchumba, kama inavyobainika katika wimbo ufuatao wa kubembeleza watoto. Wimbo uliokusanywa na C. Velten ( 1903 : 17).

Silie mama silie

Ukilia waniliza

Wanikumbusha makiwa

Makiwa ya baba na mama

Baba na mama watende

Wanioza dume kongwe

Halisafiri halendi

Kazi kumega matonge."

Mila hii imebainika katika riwaya ya Utengano wakati Maksuudi anataka kumkataza mwanawe Mussa kwa mpenzi aliyemchagua mwenyewe.

Dhana ya majaaliwa pia ni falsafa ya dini ya kiislamu (Were 1982). Kulingana na dhana hii waumini hushikilia kwamba maisha yao humu duniani tayari yamekwisha andaliwa na Mungu. Kwa hivyo yale yote yatokeayo au yanayowakumba humu duniani ndiyo maajaliwa yao. Falsafa hii huwapa waumini matumaini ya kuishi baada ya maziko na kwamba hawana budi kutambua tahadhari zinazotolewa na dini dhidi ya anasa za dunia. Imani ya dini imetumiwa katika jamii ya waswahili kuendeleza dhana ya majaaliwa ambayo huchukulia kwamba mambo yanayomkumba binadamu yanatokana na kudura za Mungu. Haya majaaliwa yaliwafanya wanawake wengi kuchukulia kuwa majukumu anayotwikwa katika jamii na shida na mateso anayoyapitia ni majaaliwa, hili liliwafanya wanawake kuteswa katika ndoa hata bila kujaribu kujinusuru, kama inavyofanyika katika ndoa ya Maksuudi na Tamima katika riwaya ya *Utengano*. Tamima anateswa lakini hataki kujinasua katika mateso haya. Kwa upande mwingine kurani inabainisha wazi usawa kati ya mwanamume na mwanamke hasa tuchunguzapo sura ya 33 aya 35; Bila shaka wanaume wenye kufuata vizuri nguzo za uislamu na wanawake wanazifuata vizuri nguzo za

uislamu..........................................na wanaume wanaomtaja Mungu kwa wingi na wanawake wanaomtaja Mungu kwa wingi anawaandalia msamaha na ujira mkubwa.

Aya hii inakariri usawa kati ya mwanamke na mwanamume , aya hii ni tofauti na dhana ya majaaliwa wanayopewa wanawake katika dini ya kiislamu.

Sembene Ousmane (1972 : 19) katika *The Money Order With White Genesis,* anasema kwamba, kwa muda mrefu jamii ya waswahili imeunda itikadi mahsusi chini ya dini ya Kiislamu na kwamba hata zile zinazobainisha kujamiana kwa watu wa akraba moja (maharimu) zinachukuliwa kwamba zimepangwa na Mungu, mwandishi anaisawiri hali hii kupitia kwa Diole anayemnajisi Bintiye na kuingiza majaaliwa.

Utawa ni njia nyingine inayotumika na wanaume chini ya kivuli cha dini ya Kiislamu .Kuhakikisha kwamba wanawake wamewekewa mipaka, katika jamii ya waswahili hii asasi imejidhihirisha, wanawake wanatawishwa kwa kufungiwa ndani ya nyumba na kushurutishwa kuvaa Hijab kila wakati wanapotoka nje , kwingineko asasi hii hujulikana kama Purda sababu muhimu za utawa ni kule kuwafungia wanawake kwa kuhofia kwamba wakiachwa huru, watatembea na kujamiana ovyo na wanaume kwa kuwa wanawake wanachukuliwa kama viumbe dhaifu. Lakini kabla ya kuchunguza chanzo cha utawa hatuna budi kuelewa jinsi dini ya kiislamu inavyomchukulia mwanamke! Katika uhalisi wake dini ilizingatia usawa baina ya mwanamke na mwanamume kupitia kurani tukufu sura ya 4:1 "Enyi watu mucheni mwenyezi Mungu ambaye amekuumbukeni katika nafsi (asli) moja na akamuumba mkewe katika nafsi

ile ile, na akaeneza wanaume wengi na wanawake kutoka katika wawili hao, na mucheni mwenyezi Mungu ni mlinzi juu yenu (anayeona kila mnayoyafanya)."

Usawa huu ulibainika nyakati za mtume Muhamed, kwani wanawake waliweza kupewa majukumu mahsusi ya umma. Historia inatuonyesha ya kwamba yale yaliyomo kwenye hadithi (Kumbukumbu zihusuzo) matendo na matamshi ya mtume Muhammad yalihifadhiwa na mmojawapo wa wake za mtume aliyeitwa Aisha. Isitoshe Fatuma aliyekuwa Bintiye Mtume Muhammad na pia mke wa Khalifa Ali, alikuwa mhubiri na mshairi mashuhuri. Hii ni ithibati muafaka kwamba wanawake wa kiislamu hawakuwekewa vikwazo vya utawa tunavyovipata sasa katika jamii nyingi za kiislamu.

Itikadi ya kuumeni iliyojipenyeza kwenye dini na kuenea katika utamaduni wa Kiislamu, Ilimchukua mwanamke kama kiumbe hatari aliyepaswa kutengwa na wanaume ili asiwaingize katika dhambi.

Katika kitabu kiitwacho *The challenge of Islam* kilichohaririwa na Gauhar (1978 – 267) mwandishi wa makala haya Aisha lemu, anaeleza kwamba chanzo cha utawa kinatokana na maandiko katika kurani sura 33 : 32 – 33. "Enyi wanawake wa mtume, nyinyi si kama yeyote katika wanawake wengine .(Nyinyi wakeze mtume)...kaeni majumbani mwenu, wala msionyeshe mapambo yenu kama walivyokuwa wakionyesha mapambo zao wanawake wa zama za ujahili..."

Katika uhalisia wake utawa uliwahusu wanawake wa akraba ya mtume Muhammad, lakini baadaye chini ya taathira za kiajemi, desturi hii ilienea na kusambaa kote katika ulimwengu wa kiislamu, (Stobel 1979) kulingana na haya basi, itikadi ya kwamba, mwanamke ni kiumbe hatari anayepaswa kutawishwa ilienea, kwa hivyo pale

ambapo kurani ulihubiri usawa, jamii za kiislamu ziliteua asasi ya utawa chini ya kusingizio cha dini ili kumwekea mwanamke mipaka.

Katika dini ya kiislamu ndoa rasmi huidhinishwa na kadhi, khatibu ama mwalimu wa dini, hata hivyo mbali na ndoa hii, jamii ya waswahili imebainisha pia ndoa ya siri na usuria. Ndoa ya siri ilihusisha kuweko kwa arusi lakini bila kuwajulisha jamaa, hasa wale wa upande wa mke, iwapo anayeoa tayari ana mke mwengine ama wake wengine huu ndio ulikuwa usiri wa ndoa hii, kwa hivyo mke na jamaa zake waliweza kujulishwa baada ya ndoa hii, usuria haukuambatana na sherehe zozote, hata hivyo ilikubalika kisheria. Uke wenza unakubalika katika jamii hii na uliidhinishwa na dini. Katika kurani sura 4 :3 Na kama mkiogopa kutowafanyia uadilifu mayatima,basi ogopeni vile vile kutowafanyia uadilifu wanawake. Basi oeni wanaowapenda katika wanawake, maadamu mtawafanyia irisafu, wawili au watatu au wane tu. Na mkiogopa kuwa hamwezi kufanya uadilifu, basi oeni mmoja tu…

Tunapochunguza kurani 4:129 mwanamume ametahadharishwa dhidi ya kuoa wake ambao hawezi kuwatunza kwa usawa bila mapendeleo, Hii ina maana kuwa manyanyaso ya wanawake yapatikanayo katika ndoa, hayalingani na mafunzo ya dini ya kiislamu. Mwanamume anatambua kwamba ana uhuru wa kidini kuoa wake hadi wane, lakini tuchunguzapo katika jamii hii mume kutoa talaka ni jambo Linalotokea kwa urahisi mno, mume hujipa uhuru wa kumtaliki mkewe wakati wowote bila taarifa, aghalabu bila hata kufuata sheria za dini zilizowekwa (Taz kurani sura 2 : 229).

Wanawake ambao kwa kawaida hawana nguvu za kiuchumi hujibidiisha mno kuwatumikia waume zao ilimuradi wasipewe talaka. Isitoshe, ni wazi kwamba ndoa za

waswahili waislamu hushirikisha zaidi ya mke mmoja panapotokea haja Momanyi 1998, Knappert 1967 : 58), kwa mfano anasema ni rahisi sana kwa mume kumtaliki mkewe kama ilivyo rahisi kumfuta kazi mtumishi, kwa mwanamke ni vigumu sana kumpa mumewe talaka hata hivyo lazima apate kibali cha mumewe ijulikanayo kama fasikhi iwapo mume huyo amemtupa mwanamke pia hupata ruhusu ya kutoa takala twayo khuluu ambayo mke humlipa mumewe malipo aliyotoa wakati wa arusi yao. Talaka ya aina hii haiwezi kubadilishwa. Momanyi 1997 anaeleza kuwa baadhi ya wanawake aliwahoji Mombasa na Lamu ilibainika kuwa kulingana na desturi mwanamke hapaswi kumtaliki mumewe, hii kwa kweli ni itikadi iliyoendelezwa na jamii ya waswahili kwani kurani haibainishi jambo hili. Jamii hii ilifanya hali ya wanawake kutoa sadaka kuwa ngumu sana ili wanaume waweze kuwamiliki wapendavyo hii ni itikadi ya kuumeni inayosingizia dini ya kiislamu.

Momanyi (1998) wakati wa mtume Muhammad wanawake waliweza kuwakataa mabwana zao bila vikwazo anaeleza kuwa mtume Muhammad mwenyewe aliwahi kukataliwa mara tatu na wake zake.

Kulingana na yale yaliyojadiliwa itikadi kadha za waswahili hazina uhusiano na dini ya kiislamu, kwa mfano itikadi zinazohusu asasi ya ndoa kinyume na ndoa halisi katika dini ya kiislamu.Katika ndoa hizi mwanamume amejijengea uungu akajinasibishe na Mungu hususan katika kutoa uamuzi wa hatima ya mwanamke, Itikadi kama hizi humfanya wanamke Kumnyenyekea mwanamume zaidi kama Mungu.

### 3.2. Athari za dini ya Kiislamu katika ndoa katika riwaya ya *Utengano*

Maksuudi ambaye alikuwa mchochole mwanzoni, alijitokeza kama mtetezi wa haki na kiongozi shupavu, mpaka dakika ya mwisho. Maksuudi anajifanya "mtaalamu, kasoma

dini sana, na ni mcha mungu, atakuwa na ngao kubwa ya kufichia utashi wake" uk 17) watu walimwamini kwa msimamo wake hadi wakampa uongozi.

Kwanza jumba la Bwana maksuudi linatambulika kama "kasri la watawa" (uk19) zaidi ya wale watumishi wake wanaoruhusiwa kuingia na kutoka waliobaki walikuwa watawa. Na hawa hasa ni wawili Bi Tamima, mkewe, na maimuna Bintiye" Uisilamu ambao maksuudi anajidai anauelewa hautarajii mwanamke kutawishwa, hizi tu ni itikadi za waswahili na hazina uhusiano na dini ya kiislamu.Maksuudi anazingatia kuwa mwanamke ni kiumbe hatari anayepaswa kutawishwa, kwa hivyo pale ambapo kurani ilihubiri usawa, jamii za kiislamu ziliteua asasi ya utawa chini ya kisingizio cha dini ili kumwekea mwanamke mpaka kama anavyofanya maksuudi kwa kuwekea mkewe na mwanawe wa kike mipaka "... Isipokuwa Bwana Maksuudi ambaye kama si kuwa leo ni jumapili ya mwisho wa mwezi, angalikuwa amebaki peke yake, ama saa hizo, na taa zake za thurea ghorofa ya tatu zingalionekana kuwako usiku huu wa manane kumwashiria yeyote aliyepita chini kuwa bwana maksuudi alikuwa yu macho na kwa mbali kama angalitega sikio angalisikia sauti iliyojaa madaha ikiteremka kwa maghani ya nyuradi alizokuwa akizisoma saa ya ibada" Maksuudi amejitokeza kama muumini wa dini ya kiislamu, kwa kuwa na ibada maalum ya waislamu anayoifanya kwa kusoma dua fulani na kumtaja Mungu (Uradi) nyumbani kwake, lakini matendo yake yanakuwa kinyume na mafundisho ya dini ya kiislamu. Uk 19" lakini leo katika jumba hili Bwana Maksuudi ameshatoka .na hii ilikuwa kawaida kwake. Jumamosi kuamkia jumapili ya mwisho wa mwezi lazima maksuudi atoke akalale pahala Fulani, au kama alivyosema mwenyewe, akafanye ibada kwenye kaburi la shehe wake.

Inabainika wazi kuwa maksuudi anatumia dini ili kuenda kwa kazija ambaye ni kimada aliyemweka kisiri, ingawa ukewenza unaidhinishwa katika dini ya kiislamu, kisichokubalika ni kujamiana na wanawake mtalaka au kahaba na hili ndilo Maksuudi analoliendeleza.“...babako hataki tutoke nje ila kwa ruhusa yake, na humu asiingie mtu ila kwa ruhusa yake bi Tamima alimeza maumivu. Huu ni uoga aliouingiza maksuudi ndani ya mkewe, dhuluma hii inaendelezwa kwa mwanamke kinyume na mafundisho ya dini ya kiislamu yanayohubiri usawa.

> "Mimba ya kwanza Tamima alizalia nyumbani
> ya pili nyumbani, na hii ya tatu ndiyo haina
> mkunga wala daktari" Uk 21.

Kama anavyosema Mbatiah (1994) dini imetumiwa na wanaume kumdhalilisha na kumdunisha mwanamke katika maisha ya ndoa, anaendeleza kuwa pamoja na dini na utamaduni, ukosefu wa elimu humfanya mwanamke mbumbumbu katika jamii. Hili linabainika wazi kwa mwanamke huyu ambaye anahatarisha maisha yake kwa kumwogopa mumewe.

katikaUk 26.

> "mbona mapenzi au ndoa ya babake na mamake ni
> ndoa ya mateso, na mateso yenyewe ya upande mmoja?
> Anayeteswa ni mamake tu.
> Na hivi alikumbuka uchungu wa mamake."

Hertinger (1979) anatueleza kuwa kwa sababu ya dhuluma zinazowakabili wanawake kama zile za kutokuwa na uhuru, wanakuwa na matatizo mengi ya kihisia na kiakili kuliko wanaume naye Engels (1844) katika Ndungo anasema kutojitegemea kwa

mwanamke ndiko kunamfanya anyanyaswe, aonewe, adhulumiwe na adunishwe kama anavyofanywa bi Tamima na mwanawe wa kike.

> "wewe ni wa kufungwa ndani kama kuku? Huyo kuku
> Ana afadhali. ikitaka iwe zama za utumwa, na sasa utumwa
> huo wa kutawishwa umekwisha na hapo zamani, bwana
> akitawisha suria wake, si mwanawe"

Katika ukombozi wa mwanamke Wollscraft (1972)anasema kuwa elimu ndiyo msingi wa kila kitu maishani na kukosa elimu ni kukosa kitu cha thamani kubwa sana katika maisha,anaendelea kueleza kuwa elimu ndiyo inaweza kumfanya mtu ajielewe,aielewe jamii na kupata kazi nzuri. Katika riwaya ya Utengano mwanamke amenyimwa elimu,ukweli huu unadhihirika kupitia kwa familia ya bwana Maksuudi, yeye anamsomesha mwanawe wa kiume, Mussa hadi Chuo Kikuu ilhali anamtawisha na kumnyima elimu mwanawe wa kike yaani Maimuna,hili linamfanya Maimuna akose kujielewa na hata mwishowe anapotoroka nyumbani anakosa kupata kazi nzuri, anaishia kupata kazi katika vilabu vya pombe na kufanya kazi ya ukahaba kwa kuwa,hakuwa na elimu, naye nduguye wa kiume Mussa anaishia kupata kazi ya udaktari kwa sababu ya elimu aliyopewa na bwana Maksuudi. Ingawa Maksuudi anajifanya mfuasi sugu wa dini ya kiislamu anaenda kinyume na mafundisho ya dini hiyo;Kurani tukufu sura ya 33 aya ya 35 waislamu wanafunzwa kuhusu usawa wa kijinsia.

### 3.3.Matatizo yanayowakumba wanawake katika riwaya ya *Utengano*

Katika riwaya ya Utengano tunaambiwa;

> "...Farashuu alisimama tulii, nadhari yake ikatunga pahali
>
> Pamoja.Kwa meza kulikuwa na picha kubwa ya mwanawe,

Mwanasururu.Huyu ameshatengana na ulimwengu,amekufa

Kabla siku zake.Na Maksuudi, huyu Maksuudi ndiye, ndiye aliyekuwa

Sababu ya kifo chake. Na ile mali ya mwanawe.......yote

Imefilisishwa na huyu Maksuudi.........Anakumbuka alipomhadithia

Jinsi yeye Mwanasururu alipigwa kanda mpaka akazirai."

Kutokana na yale ambayo tunayapata katika nukuu hii,inabainika wazi kuwa asasi ya ndoa hii ya Maksuudi na mkewe wa kwanza Mwanasururu ilikumbwa na mateso mengi, hii ndoa kulingana na madhehebu ya dini ya kiislamu inaitwa ndoa ya Mut'a ambayo ni batili, hii ni aina ya ndoa ya mtu kutaka kuoa mwanamke kwa muda maalum tu, kisha amwache, kwa mujibu wa madhehebu ya kiislamu ndoa za namna hiyo si sahihi na Ikdi haifungki, alivyofanya Maksuudi ya kumfilisisha Mwanasururu ni kinyume na mafunzo ya dini ya kiislamu kuwa, hata kama mke ni tajiri, hata hivyo masrufu hayatatoka katika mali yake,mumewe hawezi kabisa kuyatumia hata kuyashika maadamu mke mwenyewe hataki; *Ndoa na Talaka*(uk19). Baada ya kuachana na Mwanasururu Maksuudi anamuoa Bi. Tamima,tabia hii yake ya kuwadhulumu wanawake inaendelea kudhihirika wazi kwa ndoa yake na Tamima.

"....Hii talaka,Maksuudi alimtupia Tamima ile karatasi aliyokwisha

Iandika.Tamima alinyoosha mkono na kuiokota talaka yake... "

Katika *Ndoa na Talaka* (24)tunaambiwa kuwa,Lakini inatakiwa ijulikane kuwa ingawa jambo hilo la talaka linahalalishwa,kukubaliwa na kuruhusiwa na sheria, bali ni jambo lenye kumchukiza mwenyezi Mungu na Mtumewe.Na huko kuchukizwa kwake ni kwa

ushahidi wa kisa cha Mtume S.A.Waliposema "Katika halali za kumchukiza mwenyezi Mungu ni talaka "kisa hicho cha Mtume S.A.W Kinaonyesha kwamba kuachana si jambo la kupendeza katika sheria za dini ya kiislamu na kwamba jambo hilo hufaa tu ikiwa hakuna budi.

Rodney(1972)anatueleza kuwa wanawake walidhulumiwa katika taasisi ya ndoa dhuluma ilikuwa kati ya mwanamume mmoja na wanawake wengi.wanaume wenye mashamba makubwa na mifugo wengi walioa wake wengi ili waweze kupata wafanyakazi wa mashamba hayo haya ya Rodney yanashabihiana na tabia za wanaume sabuli ya Maksuudi, kwa kuwadhulumu wanawake wengi,kwanza Maksuudi anamdhulumu mwanasururu kwa kumhini mali yake na hata kusababisha kifo chake, pili anamnyanyasa mkewe kwa kumpiga, kumtawisha na kutokuwa mwaminifu katika ndoa mwishowe ana mpa talaka mkewe na hata kumnyang'anya kitoto chake kichanga, hili linasambaratisha familia ya Maksuudi, mwishowe anamnyima mwanawe wa kike haki ya kupata elimu na uhuru ili linasababisha kutoroka kwa Maimuna na kuishi maisha ya taabu.

> "Bi.Kazija anadokeza kwamba,anamchukia mwanamume kwa sababu dhahiri kuwa amewekwa mbele,ingawa hajui ni nani aliyemweka mbele huyu mwanamume, pili,Kazija anaichukia nafsi yake iliyolemaa na kuridhi siku zote kumpembejea mwanamume ambaye ni kiumbe kama yeye.Kazija anachukia hali yake,anachukia jamii yake,anachukia kila kitu.Kazija anashughulika kujipamba kwa ajili ya kumfurahisha mwanamume,yeye anachukia kujipamba kwa ajili ya kumvutia mwanamume,anachukia haya yote lakini atafanyaje."

Engels (1844)katika Ndungo(1989)anatuelezea kwamba kutojitegemea kwa mwanamke ndiko kunakomfanya anyanyaswe, aonewe, adhulumiwe na adunishwe,haya maelezo ya Engel yanadhihirisha wazi anayoyapitia Kazija kwa sababu ya kutojitegemea kiuchumi, inabidi afanye hata mambo anayoyachukia ya kumbembejea mwanamume ili asaidike. Naye Woolf (1929) analipa uzito swala la uchumi kwa ukombozi wa aina yoyote hata wa mwanamke,anadai kuwa mwanamke hawezi kupata ukombozi wowote kama hajakombolewa kiuchumi. Ingawa wanawake kama akina Kazija wamegundua kuwa wanadhulumiwa na mwanamme hawana la kufanya kwa sababu hawajakombolewa kiuchumi kazi yao itakuwa kulalamika tu. Katika jamii zote ulimwenguni hata hii ya akina Kazija ikiwemo nyenzo zote za kuzalisha mali zilitawaliwa na mwanaume huku wanawake wakiwa wategemezi na watumishi wa wanaume, hali hii huwakumba wanawake kwa sababu tangu zamani wamenyimwa nafasi ya kujiendeleza kiuchumi.

Kwa kawaida maisha ya binadamu hutegemea uchumi, hali ya binadamu ikiwa mbaya hali ya maisha yake huwa pia mabaya walio na uwezo kiuchumi wanatumia nguvu zao za kiuchumi kwa kuwatawala na kuwanyanyasa wengine. Haya ndiyo yanayotokea katika maisha ya Kazija, yeye hawezi kujikomboa kwa sababu hana nguvu za kiuchumi, haya hayampati tu kazija pekee, katika riwaya ya Utengano wanawake wengine wanadhulumiwa na bwana maksuudi kwa kukosa kujitegemea kiuchumi. Kazija anasema;

> "Na kwa kweli yeye hafanyi laana
> Kwa kupenda,ila ni kwa sababu
> Ya ukosefu."

Kazija inatudhihirishia kauli kuwa ukombozi wa mwanamke unategemea kujikomboa kiuchumi kwanza. Biti Kocho asema;

"Ulimwengu umeshanifanya kubwa zaidi
Hilo kunileta kwako nikakwangura maadishi
Kwa kupata tonge.Nimekosa nini mimi hata
Nikawa mtumishi wako? lipi kubwa zaidi
Litakaloshutua mimi kuliko unyonge
Niliozaliwa nao? "

Biti kocho katika kauli yake anatubainishia kuwa umaskini ndio ulimpeleka kufanya kazi kwa Maksuudi. Biti Kocho anamkejeli Tamima kwa kusema,

"Tamima we,usiye mbele wala nyuma, tekeleza amri
Za bwana upate muradi wako."

Tamima alifunga kidemu kutekeleza suna na faradhi za ndoa lakini wapi, Maksuudi aliguna na kumpa talaka. Knappert (1967) kwa mfano anasema ni rahisi sana kwa mume kumtaliki mkewe kama ilivyo rahisi kumfuta kazi mtumishi, hili linatokea wakati Maksuudi anapoamua kumfuta kazi mtumishi wake Biti Kocho na kwa hali hiyo hiyo kumpa mkewe talaka.Knappert anaendelea kusema kuwa,kwa mwanamke ni vigumu sana kumpa mumewe talaka, akitaka kumpa talaka ni lazima apate cha mumewe kijulikanacho kama Fasikhi iwapo mume huyo amemtupa.

Ndoa kati ya Selume na Shoka imekumbwa na matatizo mengi inabainika kuwa Shoka hatekelezi majukumu yake ya kuitunza familia yake; katika uk(112)"Niache nibebe mizigo nisiyostahili kuibeba. Na kama wewe mwanamme kweli, toka usirudi tena kuja kula alichokichuma mkeo. Lo, huna haya wewe, ungalikuwa unazo, usingalikula chakula

usichokijua kinakotoka. Lo, yasini! Selume alikuwa akitetemeka kwa hamaki, ari na majuto. Ghadhabu ndizo zilizompa aseme maneno hayo na utumwa, unyonge, na manyanyaso ya mwanamme. Mwisho wa maneno yake daima ulikuwa, "Tumo taabuni wanawake. Huu utumwa kamili. "Lakini hakujua ni namna gani alikuwa mtumwa.Alijiona anafuata kawaida na kanuni za iliyotoka mbali ambayo imekuwa ngumu kugeuka. Haijulikani mila,au jambo gani. "Kilio hiki cha Selume kinatuonyesha vile suala la ndoa linavyomdhalilisha mwanamke nao wanaume kama Shoka wakiendeleza dhuluma hizi.

Mwanamke pia amesawiriwa kama kiumbe cha kumfurahisha mwanamke ndiposa wanawake kama mama Jeni na Biti Sururu wanawatumia wanawake wadogo kati madanguro yao ili wawavutie wanaume.

### 3.4 Hitimisho

Katika sura ya tatu tumetathmini mtazamo wa dini ya Kiislamu kuhusu ndoa kama unavyosawiriwa katika riwaya ya *Utengano*. Pia tumeyaangazia matatizo yanayowakumba wanawake katika riwaya ya *Utengano*.

# SURA YA NNE

# HITIMISHO

## 4.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia matokeo ya utafiti wetu na njia zilizotumiwa katika kufikia matokeo haya. Utafiti huu wetu unadhamiria kuchunguza nafasi ya dini katika ndoa katika riwaya za *Paradiso* na *Utengano*.

## 4.1 Hitimisho

Katika kazi hii tumetumia nadharia mbili ambazo ni Ufeministi wa Kimarekani na Ufeministi wa Kiislamu. Tumezingatia Ufeministi wa Kimarekani kwa kuihakiki riwaya ya Paradiso ambayo imejengwa kwa msingi wa dini ya Kikristo, tunataka kusawiri mtazamo wa jamii unapoingiliana na mtazamo wa kigeni kuhusu dini. Mwandishi anapaswa kusawiri vilivyo maisha ya jamii. Tutaangazia katika sura hii mahusiano kati ya dini,ndoa na mahusiano haya yanavyomhusisha mwanamke katika dini ya Kikristo, pia tutaichunguza nafasi ya mwanamke katika mahusino haya.

Katika sura ya tatu tutaihakiki riwaya ya *Utengano* kwa kutumia nadharia ya Ufeministi wa Kiislamu tumechagua nadharia hii kwa kuwa ina uhusiano na jamii ya waislamu ambayo ndiyo jamii ambayo riwaya imesawiri yetu,tunaangazia nafasi ya dini ya Kiislamu katika ndoa na pia tunaangalia nafasi ya mwanamke katika uhusiano kati ya dini ya kiislamu na ndoa.

Katika utafiti huu, mtafiti ameihakiki athari ya dini ndoa inavyojitokeza katika riwaya mbili za Kiswahili ambazo ni: *Utengano* na *Paradiso*. Kwa kuhitimisha, tataangalia kwa ufupi yale tuliyoyajadili katika sura zilizotangulia. Aidha tutaangalia

kufaulu au kutofaulu kwa waandishi hawa katika kushughulikia suala la ukombozi wa mwanamke.

Katika riwaya hizi (Paradiso na Utengano) wandishi wameyaangalia masuala kadha yanayoonyesha hali halisi ya maisha ya jamii wanayoizungumzia ambayo ni ya Kiafrika. Waandishi wamesawiri maudhui kama vile dini na kizazi kipya, dini na utamaduni, dini na malezi ya watoto na dini kama imani isiyo na mashiko.

Waandishi hawa pia wameonyesha jinsi mara nyingi utamaduni na imani za jamii husika zinavyoshinda imani za kidini na kuzionyesha kuwa zisizo na nguvu zozote zile. Waandishi wameonyesha pia kukubaliana na mawazo ya Sigmund Freud (1961) aliyesema kuwa dini ni imani isiyo na mashiko. Haya yameonyeshwa kupitia kwa vitendo vya wahusika mbalimbali. Waandishi hawa wawili wamesawiri hali ya kutamausha ya dini.Wameonyesha kuwa dini imeshindwa kuleta suluhisho kwa matatizo ya wanadamu. Masuluhisho yanayotolewa na dini hayamwelekezi binadamu katika kuyatatua matatizo yake. Dini imesawiriwa kama chanzo cha matatizo katika jamii.

Mwandishi wa Paradiso anayadadishi na kuyachunguza mambo ya dini kwa jicho la ndani. Kwa kuzingatia haya yote, ni dhahiri kuwa kulingana na waandishi hawa dini imepoteza ile nafasi yake kubwa na muhimu ya hapo awali na hivi basi wanadamu wanafaa kiijucha na kujua ni yapi mema katika imani za kidini. Msimamo wa waandishi hawa ni kwamba dini imepoteza umuhimu wake kwa kiasi kikubwa kwa sababu watu wengine katika jamii ya kisasa wameidunisha na Mungu kwa kiasi cha kujifikiria kama miungu wa kuabudiwa.

Kutokana na uchunguzi wetu tuliofanya, imebainika kuwa nafasi ya mwanamke ingali katika hadhi ya chini mno ikilinganishwa na ya mwanamume. Ingawa waandishi hawa Habwe na Mohamed wamejaribu kutuletea picha kamili ya mwanamke katika jamii na matatizo anayoyapitia kutokana na dhuluma kutoka kwa mwanamume hawa waandishi wametetereka kidogo. Kuna baadhi ya mambo ambayo hawakuyashughulikia kwa ukamilifu na hivyo kushindwa kuwaongoza wanawake ili waufikie uongozi wao.

Katika riwaya ya Paradiso mwandishi amewasawiri wanawake kama viumbe wanaowategemea tu wanaume, hata kama wanawake hawa wamesoma wanakuwa na matatizo ya kuyamuda maisha yao, mzuri ni ule wa Patricia ambaye amesoma hadi Chuo Kikuu lakini bado anahangaika na kumtafuta mwanamume ili aone maisha yake kuwa yamekamilika, pia anatumia wahusika kama Kasisi Lona kuonyesha kwamba, njia zinazoweza kuleta utulifu katika ndoa ni mwanamke akitumia mitishamba kumdhibiti mwanamume. Waaidha anaonyesha udhaifu hata wa wanawake waliosoma kama Lydia kumtegemea Michael ambaye alikuwa na kisoma cha chini. Michael anafaulu kuwateka bakunja marafiki ambao wamesoma hadi vyuo vikuu.
Mohamed kwa upande wake amewasawiri wanawake kama viumbe dhaifu ambao nia yao tu katika riwaya inaongozwa na kisasi dhidi ya mwanamume,kuna mkinzano katika usawiri wa mwanamke katika riwaya hii,kwa mfano, Kazija ameangaziwa kama mwanamke shujaa anayezijua haki zake lakini mwishowe anafanya kinyume,pia mwandishi badala ya kumjenga mhusika kama huyu anampoteza tu baada ya uwanja wa uchaguzi, Biti Kocho pia licha ya ukakamavu wake kwa kumkabili Maksuudi anapotea

tu mwanzoni mwa hadithi. Mwishowe anatuonyesha kuwa mwanamke huweza tu kuwa na utulivu akiingia katika asasi ya ndoa; kupitia kwa ndoa ya Maimuna na Kabi, ingawa Kabi ni mlemavu mwandishi anatuletea dhana kuwa licha ya upungufu wa kimaumbile mwanamume tu ndiye anayeweza kumuokoa mke.

Riwaya hizi mbili zinakuwa muhimu katika mwanga wa nadharia zetu kwani zinagusia baadhi ya vipengele muhimu ambavyo vinaweza kushughulikiwa ili kuchochea mapinduzi miongoni mwa wanawake,lazima zijaribu kumfafanua mwanamke ambaye ni kiumbe anayestahili kuigwa kwa kuwa ameshaupata ukombozi wake.

## 4.2 Mapendekezo

Mtafiti anapendekeza kuwa tafiti za baadaye zichunguze pia nafasi ya mwanamume katika dini na asasi ya ndoa katika riwaya ya Utengano na Paradiso na pia kazi zingine za Fasihi kama tamthiliya, na ushairi.

Utafiti wa baadaye unaweza kuchunguza iwapo nafasi ya mwanamke imebadilika hasa baada. ya kupata elimu, kuajiriwa kazi na mengineyo. Itabainika kama ugawaji wa majukumu umebadilika au la, na hasa jamii ya waswahili, waumini wa dini ya kiislamu. Tafiti za baadaye pia ni vyema zichunguze kama mahusiano ya kidini yamebadilika kwa sababu ya wanajamii kupata elimu kwa wingi au yangali finyu.

Aidha, mtafiti anapendekeza kubuniwa kwa nadharia mpya na mahsusi itakayoongoza uhakiki wa masuala ya wanawake. Sababu yake ni kuwa, nadharia ya ufeministi ingali na utata mwingi mno.

Tungependekeza kuwa riwaya hizi mbili zitathaminiwe kwa kutumia nadharia ya Udenguzi wa kifeministi, Usasa na Usasaleo nk. Hii ni kwa sababu kazi hizi kwa kiwango Fulani zimeegemea zaidi katika nadharia hizi. Waandishi wa kazi hizi wamedadisi misingi ya miundo ya kijamii, kidini kimaadili na itikadi za kijadi kuhusu mwanamke kama kiumbe.

Kutokana na mipaka na wakati tuliokuwa nao wa kuandika tasnifu hii, tumejibana zaidi katika mambo muhimu yanayojitokeza wazi kuhusiana na dini na nafasi ya mwanamke katika riwaya hizi. Hivyo basi tungependekeza watafiti wengine wazifanyie kazi hizi tahakiki kwa undani zaidi na kuhakikisha kuwa hakuna yaliyoachwa nyuma ambayo waandishi walitaka kuyapitisha katika dhamira, maudhui na fani zao.

# MAREJELEO


Allen, J.W. (Mh) (1971) *Tendi*, Nairobi: Heinman Education Publishers.

Clayton, R.R (1978) *The Family, Marriage and Social Change.* Lexington, Toronto: D C Health and Co.

De Beauvoir (1949) *The Second sex.* London Book Publishers.

Durkheim, E (1957) *Professional Ethics and Civil Morals* London C.J. Routledge & Paul.

Forster, E.M (1927) *Aspect of the Novel.* London. Penguin Books.

Freud, Sigmud (1961) *The Future of an I llusion* New York: w.w. Norton

Habwe, J. (2005) *Paradiso.* The Jomo Kenyatta Foundation.

Harris, W. H. and J.S. Levey (Ed) (1975) *The New Columbian Encyclopedia.* Columbia: Columbia University Press.

Karanja, E.W. (1996) "Nafasi ya Dini Katika Jamii ya Kisasa" Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Katerega, D.B. (1984) "Teaching on The Status of Women in Islam" The Islamic Journal.

Lugano, R. (1989) Usawiri wa Wanawake Katika Riwaya za Euphrase Kezillahabi, Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (haijachapishwa).

Maina, V (2005) "Nafasi ya Mwanamke Katika Tenzi Mbili za Shaaban Robert – *Utenzi wa Hati na Utenzi wa Adili*" (Tasnifu haijachapishwa).

Momanyi, C. (1998) "Usawiri wa Mwanamke muislamu katika jamii ya Waswahili kama ilivyobainika katika ushairi wa Kiswahili" Tasnifu Ya Ph.D. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Tasnifu haijachapishwa).

Mogere, O.G (2003) Uhakiki wa Riwaya ya Ahmed Mohamed katika Misingi ya Kifeministi, Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (haijachapishwa)

Mohamed, S.M (1980) *Utengano* Oxford University Press.

Mwita, L.C. (2003) Mwongozo wa Walenisi. Nairobi: Africanwide Network.

Njogu na Chimera (1991) *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K (1997) *Uhakiki wa Riwaya Za Visiwani Zanzibar.* Nairobi University Press.

Mbatiah, M (2000) *Kamusi ya Fasihi,* Nairobi; Standard text books Graphics and Publishing.

Mdee, J.S. (Mh) (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu Nairobi:* Oxford University Press.

Mlachi, S.A.K (1984) Riwaya za Visiwani (1970-180) na Ujenzi wa Jamii Mpya. TUKI.

Ndungo, C.M (1985) Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria, Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi, (haijachapishwa).

Ogundipe, L (1994) *Re-Creating Ourselves: African Women and Critical Transformation,* New Jersey: Africa World Press Inc.

Osoro, G (2003) "Uhakiki wa Riwaya za Said Ahmed Mohamed kwa Misingi ya Kefeministi." Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Tuttle, L (1986) *The Encyclopedia of Feminism.* London: Arrow Books.

Wamitila K.W (2002) *Uhakiki wa Fasihi; Misingi na Vipengele vyake* Nairobi Phoenix Publishers Limited.

Wamitila, K.W (2007) Mwongozo wa Mwisho wa Kosa. Nairobi. Vide-Muwa.

Webster,R (1990) *Studying Literary Theory. An Introduction.* London: Edward Arnold.

Wollstonecraft,M (1972) *A Vindication of The Rights of Women.* Harmondworth, Penguin. Blackwell Publishers.

Woolf, V (1929) A Room of One's Own, The Hugard Press London.